
SportPesa
TZS. 783,781,040
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SABAYA adaiwa kumiliki genge la uhalifu, silaha**


BUFE
Hili la vyumba vya madarasa kamwe tusilifanyie mzaha
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Nipashe
Mradi wa bil. 1.6/- unaohamisha wasichana kutoka umasikini
Kilimo shadidi 'kinavyowatoa' walima mpunga vijana, hadi bodaboda mtaani
• 'Haijapata kutokea' Mvomero gunia 10 hadi 45

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Desemba 17, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580797

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Mwalimu anavyoishi darasani




UKURASA 2

Mwalimu (kushoto) akieleza jinsi anavyoishi kwenye moja ya madarasa kwa kukosa nyumba ya kuishi.

UKURASA WA 4

## WIZARA YATOA WARAKA SHULE KUKIUKA MIONGOZO



WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa waraka kwa shule zote nchini za msingi...

UKURASA WA 7

## JUMUIYA YAHAMASISHA CHANJO YA CORONA

JUMUIYA ya Waislamu ya Madhehebu ya Ahmadiyya imesema inaunga mkono juhudi za serikali kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya UVIKO- 19...

## Ujerumani yasaidia vifaa vya mabilioni corona

UKURASA 4

# Mtazamo wa wadau Rais kuifumua Wizara ya Afya

UKURASA 2



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba (katikati) akiwa na Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri anayeshughulikia masuala ya Rais wa Abu Dhabi, Sheikh Mansour bin Zayed Al Nanyan (kulia), mjini Abu Dhabi, Falme ya Nchi za Kiarabu. Kushoto ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Fedha na Mipango) Zanzibar, Jamal Kassim Ali, Ikulu ya Abu Dhabi. **Habari Uk. 8. PICHA: BEN MWAIPAJA**

MICHEZO NABI : HATUACHI KITU MSIMU HUU UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Wataalamu wa magonjwa ya moyo na wazibuaji wa mishipa ya damu ya moyo wa Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) wakimfanyia mgonjwa upasuaji mgumu wa kuzibua mshipa wa moyo uliokuwa umeziba kwa asilimia 99, hivyo kushindwa kupitisha damu vizuri kwa njia ya tiba mtandao (Telemedicine). Wataalamu wa Shirika la Madaktari Afrika waliopo Hospitali ya Central jimbo la Virginia nchini Marekani walikuwa wanatoa maelekezo ya jinsi ya kuzibua mshipa huo kwa wenzao wa JKCI waliopo nchini. **PICHA: JKCI**

# Mwalimu anavyoishi darasani

**Na Anjela Mhando, SIHA**

MWALIMU wa Shule ya Msingi Lemosho iliyoko eneo la West Kilimanjaro wilayani Siha, Stephano Nyambuyu, anaishi darasani kwa takriban miezi miwili sasa baada ya Mwalimu Mkuu wa shule hiyo kudaiwa kuifunga nyumba aliyopaswa kuishi mwalimu huyo.

Kadhia hiyo ilibainika jana baada ya Kamati ya Utekelezaji ya Jumuiya ya Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Wilaya ya Siha kutembelea na kukagua mradi wa ujenzi wa matundu 12 ya vyoo unaoendelea.

Kabla ya Mwalimu Nyambuyu hajaanika madhila hayo, Mwenyekiti wa UVCCM wilayani humo, Yohana Lengere, alitoa nafasi kwa walimu wa shule hiyo kueleza kero zinazowakabili na ndipo mwalimu huyo akafichua ukatili huo.

Akisimulia ukatili aliodai kufanyiwa na mkuu wake wa kazi aitwaye Asantaeli Sandewa, Nyambuyu alidai: "Nimehamia hapa Lemosho nikitokea Wilaya ya Ngara (Kagera) baada ya kubadilishana kituo cha kazi na mwalimu mwingine.

"Tangu nimekuja katika shule hii, ninaishi darasani, Huu ni mwezi wa pili sasa na kuna nyumba ambayo mwalimu mwenzangu alikuwa akiishi imefungwa na hakuna anayeishi mle.

"Nilimweleza mwalimu mkuu anipe nyumba hiyo iliyofungwa nikae. Mkuu wangu amekuwa hanielewi, amekuwa akinijibu 'hiyo nyumba hutakiwi kuingia, endelea kujibana uishi hapo hapo darasani'."

Kwa mujibu wa Mwalimu Nyambuyu, amekuwa akiishi darasani kwa miezi miwili sasa huku akiwa hana sehemu ya kupikia na mvua ikinyesha, anashindwa kupikia nje na kulazimika kulala pasina kupata chakula.

Akionyesha kutoridhishwa na hali hiyo, mwalimu huyo aliieleza kamati hiyo kwamba: "Kwa vile ni mkuu wangu wa kazi na ni mkubwa, imenibidi ninyamaze.

"Wanafunzi wamekuwa wakichungulia sehemu ninayoishi darasani. Kwangu ni fedheha kubwa kwa sababu wanafunzi hao hao ndio ninaowafundisha."

Mbali na kuishi darasani, kamati hiyo ilibaini kuwa choo anachotumia mwalimu huyo kiko mbali na darasa hilo. Kamati hiyo pia ilibaini nyumba ya mwalimu inayodaiwa kufungwa ina choo, jiko na stoo.

Alipoulizwa kuhusu suala hilo, Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, Shaban Hassan, alikiri kuwa na taarifa tatizo za mwalimu huyo anayeweka makazi darasani. "Ni kweli hapo nyuma kulikuwa na mwalimu anaishi katika nyumba iliyofungwa lakini kwa sasa mwalimu huyo alishaondoka. Siyo sahihi mwalimu kuishi darasani, tutafanya utaratibu mwalimu huyu apewe nyumba.

"Kwenye ile nyumba walikuwa wanakaa walimu wa kike wawili na mmoja amehama, amebakia mmoja. Tutafanya utaratibu huyu mwalimu wa kike, tumhamishe akae na mwalimu mwenzake wa kike na mwalimu aliyekuja ni mwalimu wa kiume, naye apate sehemu ya kuishi," alisema.

Alipotafutwa kwa njia ya simu kutoa ufafanuzi kuhusu madai dhidi yake, Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Sandewa, alidai mwalimu amewadanganya wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UVCCM kwa kuwa nyumba hiyo haijafungwa.

"Hiyo nyumba anakaa mwalimu ambaye ni mke wa mtu na yuko likizo. Sasa haiwezi kuwekwa mke wa mtu na mume wa mtu kwenye nyumba moja. Kuna utaratibu wake, lakini nipo njiani naelekea shuleni hapo. "Nimeshaongea na mwalimu anayeishi hapo amesema nimweke kwa kipindi hiki ambacho yupo likizo," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Siha, Thomas Apson, alipoulizwa na Nipashe juu ya jambo hilo alisema: "Nilikuwa sina taarifa na ndio nimelisikia sasa, ila inasikitisha sana kwamba kuna mwalimu anaishi darasani kwa miezi miwili.

"Niko nje ya ofisi kikazi lakini ninaahidi nitalifanyia kazi mara moja nikirejea kesho (leo). Nitakwenda katika shule hiyo kuhoji ni kwa nini mwalimu aishi darasani kwa miezi miwili wakati nyumba ya serikali ipo? Na kwa nini ifungwe huku mwalimu akiishi darasani akiwa hana hata sehemu ya kupikia chakula?"

# Maoni tofauti kusudio Rais kuifumua Wizara ya Afya

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema anakusudia kuifumua Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto ili kuongeza ufanisi huku wadau wakitoa maoni tofauti juu ya kusudio hilo.

Kiongozi huyo mkuu wa nchi alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akizindua Kamati ya Ushauri ya Kitaifa kuhusu utekelezaji wa ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa.

Alisema kutokana na wizara hiyo kuwa na vitu vingi, imeshindwa kutekeleza kwa ufanisi baadhi ya mipango yake.

"Unaposema afya tuu inabeba mambo mengi na kwa dunia ya sasa suala la afya lina vitu vingi sana, hivyo napanga kuifumua wizara hii ambayo ukiondoa suala la afya bado ina vitu vingi.

"Pamoja na mipango mingi, sera, miongozo na mikakati ya wizara hii, bado tumeshindwa kupata mafanikio kutokana na kuwa vitu vingi katika wizara moja, hivyo nitahakikisha kuwa naitenga wizara hii ya afya ijitegemee na pia nitamshauri Rais wa Zanzibar naye afanye hivyo ili twende sawa," alisema.

Rais Samia alisema ni matumaini yake kuwa kuigawa wizara hiyo kutaongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali ya wizara husika.

Katika serikali ya awamu ya tatu na ya nne, wizara hiyo ilikuwa ikishughulikia mambo ya afya pekee lakini katika awanu ya tano ndipo ilipoongezewa masuala la maendeleo ya jamii, jinsia, wazee na watoto, ambayo awali ilikuwa wizara inayojitegemea.

Akizungumzia uzinduzi wa kamati hiyo, alisema ili kuwainua wanawake wa Tanzania kiuchumi, mambo mengi yanatakiwa kutekelezwa.

"Wajumbe wa kamati hii wanatoka katika sekta mbalimbali ambao tumewachagua ili kutufikisha kwenye usawa wa kijinsia hasa kwenye masula ya usawa kiuchumi ambako sisi ndio tumechagua kuwa vinara," alisema.

Alisema wanawake wanafika asilimia 50 ya nguvu kazi ya taifa lakini bado ni waathirika wakuu katika masuala ya kiuchumi na kisiasa katika maeneo mbalimbali.

"Licha ya kuwa wanawake ni muhimu katika kutekeleza malengo ya dunia, bado kwa kiasi kikubwa ustawi wao kiuchumi, kijamii, kisiasa haujawekwa vyema kwenye mipango mbalimbali ya maendeleo au haijatekelezwa ipasavyo," alisema.

"Pamoja na kwamba nusu ya watu duniani ni wanawake bado sehemu kubwa ya dunia haijatoa nafasi stahiki kutumia ipasavyo nguvu kazi iwapo nguvu kazi ya wanawake itatumika ipasavyo inaouwezo mkubwa wa kuchangia uchumi wa dunia," alisisitiza.

Pia alisema wataalamu wamepiga hesabu na wamekisia kuwa nguvu kazi ya wanawake inaweza kuchangia dola trilioni 28 kwa mwaka, hivyo kuagiza kamati hiyo kusimamia na kuhakikisha ahadi za kuinua haki za kiuchumi kwa jamii hasa wanawake zinatekelezwa na malengo yake yanafikiwa.

**MAONI YA WADAU**

Kutokana na kusudio la Rais, wadau mbalimbali wametoa maoni tofauti huku wengi wakipongeza na wengine wakitaka ibaki kama ilivyo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti jana, walisema maboresho hayo ni mazuri na kwamba hata mgawanyo wa bajeti utakwenda vizuri na kusaidia kupunguza ukatili.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF), Anna Kulaya, alisema: "Hiki kilikuwa kilio chetu kikubwa kwa kipindi kirefu sasa. Hii sasa wizara kubwa sana na ina majukumu mengi. Kama itagawanywa ukatili utapungua. Maendeleo ya jamii ndiyo kila kitu."

Alisema jamii ikielimishwa vizuri ma rasilimali watu ikawa ya kutosha itasaidia ustawi wa jamii.

"Hii ina maana itaboresha afya, huduma za jamii, malezi. Hapo ndipo penye msingi wa taifa. itasaidia kupunguza ukatili kwa kiasi kikubwa,"alisema Kulaya.

Naye mwanataaluma mstaafu wa Taasisi ya Taaluma za Maendeleo (IDS) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Bertha Koda, alipongeza nia hiyo na kusema wizara ilikuwa na mambo mengi ambayo yote ni nyeti na kusababisha bajeti kutotoshelaza.

"Ilikuwa hata ikitengwa bajeti kubwa haiwezi kumudu matatizo ya wizara. Kwa maoni yangu naona ni sawa na ni jambo la busara ili kupunguza majukumu kwa wizara na kuhimili hata bajeti ikitengwa,"alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, alipongeza kusudio hilo kwa kuwa utekelezaji wake utarahisisha utekelezaji wa shughuli za kuhudumia wananchi na kuongeza uwajibikaji.

"Kwa mtazamo wa nje hata kama kulikuwa na idara walikuwa wanashindwa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kwa wakati. Ikigawanywa watatoa huduma watajua waende wapi kupata wataalamu ambao wametengwa kwa ajili ya masuala hayo,"alisema.

Naye Mratibu wa Kituo cha Usuluhishi (CRC), Gladness Munuo, alisema Wizara ya Afya inategemeana sana na Maendeleo ya Jamii kwa kuwa kuna masuala yanaingiliana ndiyo maana hospitali zina idara ya maendeleo ya jamii ambazo kwa pamoja husajili vizazi na vifo.

**•Imeandikwa na Paul Mabeja, DODOMA na Salome Kitomari, DAR.**

HABARI KITAIFA

# Sabaya adaiwa kumiliki genge la uhalifu

**Na Allan Isack,** ARUSHA

OFISA Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Ramadhani Juma (39), amedai kuwa aliyekuwa Mkuu wa wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, alikuwa akimiliki genge la vijana waliokuwa na mafunzo ya kujihami.

Akitoa ushahidi wake jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Juma alidai kuwa walibaini genge hilo kupitia taarifa za siri. Pia alidai kuwa genge hilo lilikuwa likimiliki na kutumia silaha za moto katika matukio ya uhalifu Arusha na Kilimanjaro.

Ofisa huyo ambaye alikuwa mpelelezi mkuu wa uchunguzi katika kesi ya Sabaya, alidai kuwa alipokea jalada lenye tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 90 zilizokuwa zikimkabili Sabaya. Juma ambaye ni shahidi wa 13 wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili Sabaya na wenzake sita, alitoa madai hayo mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda.

Mbali na Sabaya, washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Alidai kuwa jalada hilo lilikuwa likihusu tuhuma za Sabaya kuomba rushwa ya Sh.milioni 90 kutoka kwa mfanyabiashara Francis Mroso.

Akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Felix Kwetukia, alidai kuwa katika uchunguzi wake, licha ya tuhuma hizo, alibaini kulikuwapo na genge la vijana waliowatumia kufanya uhalifu ikiwamo kulazimisha kupewa rushwa ya Sh. milioni 90 na Mroso.

Shahidi huyo alidai kuwa washtakiwa hao, wakati wakifanya matendo ya kiuhalifu walikuwa wakitumia majina bandia kwa lengo la kuficha uhalisia wao.

Alitaja majina waliyokuwa wakiyatumia na majina halisi kwenye mabano kuwa ni General (Sabaya), Kicheche (Nyegu), Digidigi (Togolani), Mali Mungu (Mwahomange), Maliki One (Odemba), Chesa (Nathan), Folio B (Macha) na Kiiza Besigye (Sadick).

Kutokana na taarifa za siri, alidai genge hilo lilikuwa likiratibiwa na Sabaya kutekeleza matukio mabaya na lilikuwa likitumia silaha za moto.

Baada ya kupata taarifa hizo, alidai kuwa Aprili 24, mwaka huu, alikwenda kwa mkuu wake kumweleza aliyobaini na alimwomba kumwongezea nguvu kutekeleza wajibu wake kikazi.

"Nilimwomba bosi wangu (Mkurugenzi wa Uchunguzi wa TAKUKURU) kuniongezea nguvu kwa kuwa niligundua watu hao wanafanya matukio kwa kutumia silaha nzito tena za moto,"alidai.

Pia alidai kuwa Machi 8, akiwa ofisini kwake, aliitwa na Mkuu wa TAKUKURU Arusha na kumkabidhi jalada kutoka polisi akimtaka kulifanyia uchunguzi. Alidai jalada hilo lilihusu tuhuma zinazomkabili Sabaya kuomba na kupokea rushwa ya Sh. milioni 90.

"Baada ya kupokea jalada hilo, ndani nilikuta barua ya polisi ya kuhamisha jalada kutoka kwao kuja TAKUKURU ikiwa na maelezo ya Francis Mroso, aliyoandika kituo cha polisi Februari 11. Pia nikuta maelezo ya karani wa Mroso anayetambulika kwa jina la mzee Marandu na dereva bodaboda wa Mroso, Juma," alidai.

Baada ya kupitia taarifa fiche, alidai Februari 24, waliwasiliana na Mroso kufika katika ofisi za TAKUKURU Arusha kufanya mahojiano juu ya malalamiko yake.

Alidai Moroso aliwaeleza kwamba Sabaya na vijana wake walikwenda katika karakana yake wakimtuhumu anafanya biashara bila kutoa risiti na ni kosa kisheria. Pia alidai kwamba Sabaya alimweleza Mroso kuwa aliteuliwa na Hayati Dk. John Magufuli, kuunda kikosi kazi cha kupambana na wakwepa kodi Kanda ya Kaskazini.

Pia alidai alimweleza kuwa Sabaya na genge lake, walijitambulisha kwake kuwa ni maofisa wa Usalama wa Taifa (TISS) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na walimtishia kwamba asipotoa fedha hizo, watamfungulia kesi ya uhujumu au kumpoteza.

# 'Watoto wa kiume nao warudi shuleni'

**Na Rose Jacob,** MWANZA

SERIKALI imesema wanafunzi wote walioacha shule kutokana na sababu mbalimbali wakiwamo wa kiume wanatakiwa kurudi shule kama mwongozo wa serikali unavyotaka.

Kauli hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Ofisa Elimu Mkoa wa Mwanza, Martin Nkwabi, alipozungumza na Nipashe kuhusu mipango iliyowekwa na serikali kuhakikisha wanafunzi wote wanarudi shule bila kujali jinsia zao.

Alisema maelekezo hayo yanahusu vijana wote wa kike na wa kiume kupitia waraka namba tatu wa mwaka 2021 unaohusu urejeshwaji wa wanafunzi waliokatiza masomo shule za msingi na sekondari.

"Waraka ule wa serikali haubagui aina ya wanafunzi, bali unawataka wote wakiwamo wa kiume na kike waliokatiza masomo ilimradi wale ambao waliacha masomo kutokana na makosa ya jinai," alisema Nkwabi.

Sababu zilizoanishwa katika waraka huo ni pamoja na utoro, utovu wa nidhamu na ujauzito kwa watoto wa kike.

"Kuna masharti yamewekwa juu urejeshwaji wa wanafunzi waliokatiza masomo, hili la nidhamu linategemea ni aina gani, kuna makosa ambayo mwanafunzi atafanya ikiwamo ya vitendo vya jinai hao hawataruhusiwa kurudi shuleni, lakini makosa ya kawaida hususani utoro, utovu wa nidhamu, ukosefu wa sare za shule hao watapokelewa," alisema Nkwabi.

Aidha, Nkwabi alisema kuna fursa nyingine waliyopewa wanafunzi waliosoma hadi darasa la saba wakafanya mitihani na hawakufaulu, wamepewa nafasi ya kurudia.

Serikali ilitoa ufafanuzi huo baada ya kuwapo malalamiko kutoka kwa baadhi ya wazazi mkoani humo kuhusu suala la watoto wa kiume walioacha shule kwa sababu mbalimbali zikiwamo uvutaji bangi, utoro, ugonjwa na ugomvi, serikali kushindwa kuwatafutia ufumbuzi.

Wakizungumza kwa wakati tofauti baadhi ya wanaume walisema, wanapata hofu kwamba kunaweza kujitokeza ongezeko la watoto wa kiume wasiokuwa na elimu kukaa mitaani kama hawatarudishwa shule.

DERM group

NOTICE OF HOLIDAY SEASON CLOSURE

**Derm Group** wishes to inform its esteemed clients and business partners that our offices will be closed during the festive season with effect from **Friday 17th December 2021.**

The business will resume on **Monday 03rd January 2022.**

This closure will not affect our site operations in Bagamoyo, Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Songwe, Kilimanjaro, Arusha, and Zanzibar.

Any inconveniences caused are highly regretted.

We would like to thank all our clients and business partners in general for their continued patronage of our services throughout the year 2021.



DERM ELECTRICS (T) LTD — Electrical, HVAC, Security, ICT Co. tractors
SKYLINE PROPERTIES LTD
COAST CONCRETE POLES LTD
Derm Elevators
DTsmart

# Ujerumani yasaidia vifaa bil. 2.3/- corona

**Na Faustine Feliciane**

SERIKALI ya Ujerumani kupitia shirika lake la msaada la GIZ, limeisadia Tanzani vifaa vyenye thamani ya Sh. bilioni 2.3 kwa ajili ya kupambana na janga la Uviko 19.

Vifaa hivyo vilivyokabidhiwa jana kwenye ofisi kuu ya Bohari ya Dawa nchini (MSD) ni vya kumsaidia mgonjwa kupumua (ventilator machine) 55 pamoja na vifaa 5000 vya kupima wingi wa hewa ya Oksijeni kwa mgonjwa.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Mfamasia Mkuu wa Serikali na Mkurugenzi wa huduma za dawa, Daudi Msasi, alisema kuwa vifaa hivyo vimekuja wakati muafaka na vitasambazwa kwenye vituo 500 vya afya.

Alisema kamati kuu ya kuratibu ugonjwa wa Uviko-19 ndiyo watakaopanga vituo vya kupata vifaa hivyo muhimu.

"Waratibu hawa wa ugonjwa wa Uviko wao wanajua maeneo gani yana uhitaji mkubwa na wa haraka wa vifaa hivi, vitaanza kugaiwa maeneo hayo," alisema Msasi.

Aidha, alisema utaratibu wa kugawa vifaa hivyo ulishapangwa kwa kuwa majadiliano ya kusaidiwa vifaa hivyo yalifanyika tangu Agosti mwaka huu,kati ya Wizara ya Afya na shirika la GIZ.

"Vifaa hivi vimeingia nchini tangu Desemba 3, mwaka huu, leo (jana) au kesho (leo) vitaanza kusambazwa kwenye vituo mbalimbali kufuata maelekezo ya kamati ya kuratibu ugonjwa wa uviko," alisema Msasi.

Kwa upande wake, Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania, Regine Hess, alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania na nchi nyingine za Afrika katika mapambano dhidi ya mlipuko wa ugonjwa wa Uviko-19.

Alisema Ujerumani kama zilivyo nchi yingine inataka kuona watu wanaishi salama na ndiyo sababu wanahimiza watu kufuata njia za kujikinga kwa kuvaa barakoa na kuosha mikono kwa sabuni maalumu na kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, ametembelea mabanda ya nchi za Uganda, Burundi, Ethiopia na Kisiwa cha Malta kwa lengo la kujifunza namna nchi hizo zimeshiriki katika maonesho ya Expo 2020 Dubai. Masanja aliongozana na Mkurugenzi wa Diplomasia ya Uchumi, Balozi Edwin Rutageruka, Mkurugenzi wa Banda la Tanzania kutoka Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade), Getrude Ng'weshemi kutoka TanTrade na Afisa Masoko Mkuu kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Michael Makombe. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wizara yatoa waraka shule kukiuka miongozo

**Na Christina Mwakangale**

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetoa waraka kwa shule zote nchini za msingi na sekondari kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo, badala ya ukiukwaji kwa madai ya kutafuta ubora na ufaulu wa wanafunzi.

Ni hatua inayojiri wiki chache baada ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais -Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, kupiga marufuku wanafunzi kusoma saa za ziada usiku na wakati wa likizo shuleni, akisema anaunga mkono taarifa za athari kwa wanafunzi iliyotolewa na Chama cha Madaktari Tanzania (MAT).

"Kutokana na kuongezeka kwa shule zinazokiuka taratibu, wizara inatoa maelekezo haya ili kusisitiza umuhimu wa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo iliyopo. Kalenda iliyowekwa katika utekelezaji wa mitaala izingatiwe kikamilifu sambamba na nyaraka zote za elimu, anatamka Kamishna wa Elimu, Dk. Lyabwene Mtahabwa.

Waraka wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia uliotolewa Jumatatu wiki hii na Kamishna wa Elimu, Dk. Mtahabwa, ulisema ubora wa elimu katika shule unategemea namna zinavyoendeshwa bila ya kukiuka sheria zilizopo.

Anasema baadhi ya shule zinaathiri ufanisi katika utoaji elimu nchini na kwamba maeneo ambayo ukiukwaji wa taratibu unajitokeza zaidi, yanajumuisha ratiba ndefu ya masomo inayoanza alfajiri na kuendelea hadi usiku.

Ripoti kadhaa za uchunguzi zilizotolewa na Nipashe mwaka huu kuhusu mada hiyo ikiwamo ya tarehe 3 mwezi huu, ilibainisha kuwapo baadhi ya shule huendesha masomo kwa siku saba za wiki, kati ya Jumatatu na Jumamosi, madarasa yanaendeshwa kwa saa 14, kati ya saa 12:00 asubuhi hadi saa 4:00 usiku na nyingine zinaishia saa 2:00 usiku.

Iibainika katika ripoti hiyo iliyoonyesha mbinu za kuhadaa wazazi na serikali kutoka shule hizo, kwamba ratiba ya Jumapili maisha ya wanafunzi yanaanzia kanisani asubuhi na mchana wanaingia darasani hadi usiku, kinyume na Sera ya Elimu Tanzania Toleo la 2019, inayoelekeza wanafunzi kusoma kwa siku tano kwa wiki kwa saa zisizozidi nane kila siku.

Mengine anayotaja ni kuzuiwa likizo kwa wanafunzi hususani walio na madarasa yenye mitihani na upimaji kitaifa, pia shule kutoza michango kutoka kwa wazazi au walezi bila ridhaa yao.

Kamishna wa Elimu, ambaye Sera ya Elimu inampa mamlaka makuu ya usimamizi, anafafanua katika waraka wake huo ukiukwaji mwingine unahusu shule kuwapo mazoea ya kufanyika majaribio na mitihani kila mara na hata wanafunzi kupatiwa adhabu kama vile viboko visivyozingatia taratibu rasmi.

Alisema, hiyo inajumuisha suala la viongozi kutoa maagizo kwa shule na kumaliza ufundishaji wa mada zote katika muhula wa kwanza, ili wa pili utumike kwa mazoezi na majaribio, hasa madarasa yenye mitihani na upimaji kitaifa ambayo ni darasa la nne, saba na sekondari kidato cha pili na nne.

"Kutokana na kuongezeka kwa shule zinazokiuka taratibu, wizara inatoa maelekezo haya ili kusisitiza umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo. Kalenda iliyowekwa katika utekelezaji wa mitaala izingatiwe kikamilifu sambamba na nyaraka zote za elimu.

# 'Masharti yalegezwe huduma uzazi mpango'

**Na Romana Mallya,** MOROGORO

WADAU wa huduma ya uzazi wa mpango, wameiomba serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto kulegeza masharti ya upatikanaji wa huduma hizo ili kuendelea kwa kuhusisha sekta binafsi.

Ombi hilo walilitoa juzi mjini Morogoro katika mafunzo ya siku tatu yaliyoandaliwa na asasi ya kiraia Tanzania Men as Equal Partners and Development (TMEPiD) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) kuhusu huduma za uzazi wa mpango na mbinu jumuishi ya masoko.

Mkurugenzi wa TMEPiDP, Cuthbert Maendaenda alisema, serikali imedhamiria kuongeza matumizi ya huduma ya uzazi wa mpango na kupanua wigo wa upatikanaji wake.

"Miaka mingi imezoeleka kwamba mtu akitaka huduma ya uzazi wa mpango lazima aende kliniki, lakini akienda kuna watu wengine wanapata shida ya huduma, maeneo mengine vijana wako zaidi kwenye mahusiano ya kingono wanashindwa kuzifikia kwa sababu zinatolewa na watu wazima," alisema.

Alisema kama wadau wa uzazi wa mpango kwa sasa wanataka huduma hizo zipatikane kila mahali kupitia sekta zote binafsi na serikali.

"Huko nyuma hata kupata mpira wa kiume (kondomu) ilikuwa mpaka uende kliniki, lakini sasa zinapatikana hadi duka la rejareja, tunataka na huduma nyingine za uzazi wa mpango zipatikane kila mahali tena kwa wakati wote," alisema.

Maendaenda alisema vipo vikwazo vya kisera ambavyo duka la dawa muhimu haliwezi kuuza aina fulani ya dawa za kuzuia mimba.

Alisema wanataka vikwazo vya aina hiyo vitolewe ili mtu anayesafiri kilometa 20 aweze kununua anapovihitaji.

"Faida ya hii ni kuokoa muda wa watu wanaoutumia kuifuata huduma maeneo ya mbali, hakutakuwa na mtu kupata mimba isiyo tarajiwa, kupunguza msongamano kliniki na kuisha kwa dawa," alisema.

Pia alisema watu waliopo mjini wana uwezo wa kulipia huduma hizo kuliko waliopo vijijini.

"Tunajaribu kutetea mashirika ya bima kama ulivyo mfuko wa bima wa taifa na wenyewe katika huduma wanazotoa wahusishe huduma za uzazi wa mpango, yaani bima imruhusu mtu kupata huduma ya uzazi wa mpango na kusiwe na sababu ya kutoa fedha kwenda kununua.

"Mfano sasa hivi kuna kilio kikubwa cha nguvu za kiume, baba akienda kliniki wamejaa wanawake na watoa huduma wanawake, baba anaona aibu kumwambia mhudumu nguvu za kiume hazitoshi, tukiongeza wigo huduma zikatolewa pia na sekta binafsi maana yake tutaondoa mrundikano kliniki."

Alisema sekta binafsi ikiingilia italeta unafuu wa bajeti kwa serikali katika utoaji wa huduma hizo. Akizungumza katika mafunzo hayo, Meneja Utetezi wa Shirika la Tanzania Communication and Development Center (TCDC), James Mlali, alisema huduma za uzazi wa mpango Tanzania zinaridhisha, lakini bado kuna haja ya kuongeza juhudi.

Alisema taarifa rasmi za afya na idadi ya watu za mwaka 2015, 'Tanzania Demografic and Health Survey' ya mwaka 2015/16, watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango walifikia asilimia 32 kiwango ambacho ni kama theluthi.

"Taarifa zinazotokana na matumizi ya kila mwaka zinaonyesha kufikia 2020, idadi hiyo ilifikia asilimia 41 na tuna malengo ifikie asilimia 47, tunahitaji kufanya kazi zaidi ili watumiaji waongezeke," alisema.

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001:2015

# TANGAZO KWA UMMA

## UZINGATIAJI WA MATAKWA YA SHERIA KUHUSU KUTUNZA AKAUNTI YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI (VAT)

Mamlaka ya Mapato Tanzania inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wote waliosajiliwa na Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwa upande wa Tanzania Bara, kutunza Akaunti ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT Account) kwa kuzingatia matakwa ya Kifungu cha 89 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148. Akaunti hizo zinatakiwa kuwa na taarifa zifuatazo:

- Kodi kwenye mauzo kwa kipindi/mwezi husika
- Kodi kwenye manunuzi anayostahili kujirejeshea kwa kipindi husika
- Marekebisho yoyote ya kodi yanayotakiwa au kustahili kufanyika ndani ya kipindi husika

Sambamba na akaunti za VAT, walipakodi wote waliosajiliwa na VAT wanakumbushwa kutunza kumbukumbu na taarifa zote za masuala ya VAT kama inavyotakiwa katika kifungu cha 89 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148.

Wafanyabiashara wote waliosajiliwa na VAT wanakumbushwa kuzingatia matakwa haya ya kisheria ili kuepuka madhara au adhabu na hivyo kupelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji biashara na usumbufu usio wa lazima.

Kwa taarifa zaidi tafadhali tembelea ofisi yoyote ya TRA iliyokaribu na wewe au wasiliana nasi kupitia barua pepe na namba za simu kama ifuatavyo:

***Namba za Bure*** : 0800 750 075
0800 780 078

***WhatsApp:*** 0744 23 33 33

***Barua pepe :*** huduma@tra.go.tz
services@tra.go.tz

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

***Imetolewa na;***
**KAMISHNA MKUU**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Bravo Rais Samia

**JANA** Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza kusudio kuigawanya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ili kuwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watoto kutoa msukumo wa kushughulikia vikwazo.

Alisema sekta ya Afya inachukua nafasi kubwa ya Wizara kuliko nyingine, na kwamba kama itatengwa na kubaki yenyewe usimamizi wa sera na sheria utakwenda vizuri, huku akisema atamshawishi Rais wa Zanzibar, kufanya hivyo hivyo.

Kwa mujibu wa Rais Samia, pamoja na jitihada nyingi zilizofanywa, mipango na sera bado nchi haijafika inapotakiwa kufika na ili kufikia lazima kuwe na usimamizi, uratibu, utathmini na ufuatiliaji wa sera na utekelezaji wa mipango wa afya na mambo mengine.

Tunapongeza uamuzi huu mzuri ambao umekuwa ni matamanio ya wadau wa mashirika yasiyo ya kiserikali (NGO) zinazojihusisha na masuala ya wanawake na watoto, ambao waliona namna Wizara ya Afya 'ilivyomeza' idara nyingine kiasi cha kukosa nguvu.

Kuundwa kamati na kama pia itaundwa Wizara ya kushughulikia masuala hayo muhimu, ni matarajio yetu kuwa wadau wote muhimu watashirikishwa vyema kuhakikisha kuna mabadiliko makubwa.

Tunaamini kamati itafanya kazi nzuri ikiwamo kuzitazama sheria ambazo zinahitaji marekebisho, ikiwamo Sheria ya Ndoa, ambayo inakinzana kwenye umri wa kuoa na kuolewa.

Pia, tunaamini itafanyika tathmini ya kazi ya kamati hiyo kwa kupima matokeo chanya ambayo yametekelekezeka na kuisaidia jamii ya Watanzania.

Wanawake wanafikia asilimia 60 ya nguvu kazi ya kiuchumi na bado wanakabiliwa na vikwazo ikiwamo ustawi duni wa kiuchumi, kijamii na kisiasa na hakuna utekelezaji kama inavyotakiwa licha ya kwamba nusu ya watu duniani ni wanawake, hawajatumiwa vyema kuchangia maendeleo ya nchi.

Alisema Jukwaa la sasa la kizazi endelevu ni muhimu na kwamba hakuna anayeachwa nyuma na lengo namba tano la Malengo Endelevu ya Milenia (SGD) linatekelezwa, na kwa hesabu zilizopo duniani wanawake wanaweza kuchangia zaidi ya Dola za Marekani trilioni 28.

Kama ilivyo maeneo mengine duniani bado kuna vikwazo kwenye utekelezaji wa sera za kumuinua mwanamke kama kwenye afya, elimu, mila kandamizi, upatikanaji wa mitaji, teknolojia ya kurahisisha kazi, masoko, huduma na ugani, hifadhi ya jamii na unyanyasaji wa aina mbalimbali.

Rais alisema muda umefika wa kufanyia kazi kikamilifu sera na sheria zinazotungwa na mipango inayowekwa kwa ajili ya kuinua hali za kiuchumi ya kuleta ustawi wa jamii na taifa kwa ujumla.

Tunatarajia kuona mabadiliko makubwa ikiwamo Waziri, Naibu na Katibu Mkuu watakaoteuliwa kuendesha wizara hiyo kushirikiana na kamati kutambua changamoto za muda mrefu, ambazo jamii inaona zinaweza kupatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Pia, tuone mabadiliko kwenye madawati ya jinsia, idara za maendeleo ya jamii ambazo zipo kwenye halmashauri mbalimbali nchini ambazo zinahusika na jamii ngazi ya chini kabisa ili kuona mabadiliko makubwa katika ukatili wa kijinsia, uchumi, maendeleo ya kijamii na ushiriki wa wanawake kwenye ngazi ya uamuzi.

Ndiyo maana tunasema rais anastahili pongezi nyingi kwa kuona jambo hili muhimu kwa maendeleo ya nchi na kulipa uzito, ikiwamo kuunda kamati maalumu ambayo atakutana nayo hivi karibuni, na sasa picha yetu kimataifa itazidi kuwa nzuri.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Anthony Gervas, MWANZA.

# Tunashukuru maadhimisho miongo sita huru imevuka salama, tujipange na ukame

**SERIKALI** nchini chini ya mama yetu, Samia Suluhu Hassan, kwa kushirikiana na Watanzania imemaliza jukumu lake kuhakikisha sherehe za kutimiza miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika zimefanyika salama salimini.

Kila Mtanzania ama amepata au simulizi kutoka taasisi mbalimbali za umma na wazee ambao enzi zile walikuwa ndiyo vijana, namna siku hiyo ilikuwa nchi ikipata uhuru, ilikuwaje kipengele pale bendera ya mkoloni iliposhushwa na kupandishwa ya Tanganyika. Sababu ilikuwa ngumu kwa wananchi kuamini kutimizwa ndoto hiyo.

Elimu hiyo ya miaka 60 ya uhuru, inatupa mwanga wa kujua historia tulikotoka, tulipo, isipokuwa hatuwezi kujua kwa uhakika tuendako, ingawaje maisha mengine yanaendelea, nasi tuendelee kuchapa kazi na kufunga mkanda.

Kimsingi, Watanzania tunawajibika kufunga mkanda ili kazi zingine ziendelee katika kipindi kilichopo, ikiwamo mvua zinazoendelea, hasa mwakani tunatakiwa kujihadhari na ishara ya janga la ukame kama tulivyotahadharishwa, kwani mvua zilizopo ni za hapa na pale.

Watanzania wenzangu inatubidi tukae chonjo wakati tukishuhudia hivi sasa kuna yanayopanda bei sokoni kama vile bei za chakula, ikiwamo mahindi hapa kwetu Mwanza yanazidi kupanda hapa kwetu; kilo moja inafika hadi Sh. 3,000 kutoka Sh. 2000 na mchele kilo moja Sh.1,800 kutoka 1000.

Bidhaa zingine nazo zinapanda bei maradufu.

Wananchi wenzangu mijini na vijijini wengi ni maskini, tunategemea mazao kutoka shambani, lakini hali ya hewa inazidi kuwa mbaya. Hapa sasa tunajiuliza, tusio na mishahara itakuwa vipi kwetu?

Najua njaa ikiingia haina dereva wa kuizuia, walalahoi wengi tuko mjini na kuna uwezekano wa kula mlo mmoja kwa siku au kushindia uji na tukielemewa, tunalala matumbo tupu kabisa.

Wapo Watanzania wenzangu waliowahi kushuhudia njaa za watu inatimu jioni, hawana uhakika mlo dhahiri kwao ni nini siku hiyo, wengine wakila wakisukumia ugali na mboga isiyoeleweka, au kukomba mboga za majani ili siku iende.

Huenda kwa wenye mishahara wengi hawawezi kuyaona mateso ya njaa, kwa sababu wana uhakika mwisho wa mwezi kupokea walau mshiko fulani na kununua chakula kwa bei yeyote ile, licha ya bei ya mlo kupanda maradufu. Niseme, wanaoumia sana katikia hilo ni tunaowaita walalahoi au mahohehae wanaotegemea kilimo kuvuna mazao mengi na kuleta sokoni, ndiyo waishi vyema.

Ndiyo maana tunapozungumzia hali mbaya ya njaa, walio katika kada masikini ndiyo wa kwanza kuiona changamoto ya maisha na familia zao.

Nirejee, hatari zaidi inakuja mwakani kunakowezekana kukumbwa na hekaheka ya uhaba wa chakula, kwani wakulima wengi wameshindwa kulima mazao ya chakula, wanahofu hawatafanikiwa msimu ujao kutokana na uhaba wa mvua.

Kuhusu kupanda maradufu bei za mazao, hata kusababisha wananchi kuanza kila mmoja kupambana na hali yake, panatakiwa kuwapo njia mbadala wa mapema kudhibiti hali hiyo, ili tusirudie zama za nyuma wananchi kupewa misaada ya chakula mahindi 'kisado' kimoja au debe wakati hayatoshelezi mahitaji.

Wakulima nao kwa nafasi yao, wanatakiwa kutunza chakula, ikiwa ni jambo la kujifunza si kulima chakula kingi kisha wanauza akiba yote, wakiamini neema ya leo ni kama ya kesho.

Nakumbuka wakati wa njaa iloyowahi kutukuta ya mwaka 1984, watu walipanga foleni kwenye yaliyokuwa maduka ya ushirika nchini kugawiwa chakula cha msaada; unga wa njano maarufu Unga wa Yanga. Mateso yake yalikuwa makubwa, kulala njaa au kushindia uji ilibakii ndiyo 'habari ya mjini.'

Katika mikoa ya kanda ya Ziwa hususani Mwanza, wakulima hawana uhakika wa kulima mazao ya chakula kama vile mpunga na mahindi kutokana na uhaba wa mvua, ndiyo maana serikali inasisitiza walime mazao ya biashara kama pamba, choroko, dengu, mihogo na mengine yanayovumilia ukame.

Kwa angalizo la hali ya hewa ijayo, tuwe makini kudhibiti chakula kupelekewa nchi jirani, ikiwa namna ya kujihami, ama kuweka akiba zaidi.

# Wahandisi wasiosajiliwa ERB waonywa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAHANDISI wanaofanya kazi nchini bila kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Wahandisi (ERB), wametakiwa kuacha mara moja ili kuepuka mkono wa sheria.

Mwenyekiti wa ERB, Prof. Ninatubu Lema, alitoa tahadhari hiyo juzi jijini Mbeya wakati wa Mhadhara wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) uliokuwa na lengo la kujadili mchango wa wahandisi kwenye ukuzaji wa uchumi wa nchi.

Prof. Lema alisema kitendo cha mhandisi yeyote kusajiliwa na bodi, kina tafsiri kuwa anatambuliwa kuwa na sifa za kufanya kazi za kihandisi na kwamba kwa mtu ambaye hajasajiliwa, haruhusiwi kufanya au kusimamia kazi za kihandisi.

Alisema mpaka sasa nchini Tanzania kuna zaidi ya wahandisi 31,000 ambao wamesajiliwa na ERB na kwamba kati yao zaidi ya nusu ni wahandisi ujenzi na kwamba kuna baadhi ya fani za kihandisi zina watu wachache na zingine hazina kabisa.

Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia duniani, fani ya uhandisi kwenye teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT) ni muhimu kwa taifa ya kuhakikisha nchi inaendana na mabadiliko yanayoendelea duniani yakiwamo maendeleo ya kidigitali.

Alisema pamoja na umuhimu wa wataalamu hao, idadi yao ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji na kwamba hata wahandisi wa fani zingine waliopo kwa sasa ni wachache kulinganisha na mahitaji ya serikali kwenye utekelezaji wa miradi.

"Kitendo cha mhandisi kusajiliwa na bodi na kupewa leseni ni kuaminiwa kuwa una uwezo wa kufanya kazi hizo. Maana yake ni kwamba mhandisi ana elimu na uzoefu wa kufanya kazi kwa vitendo na kufanya kazi hizo bila kusajiliwa ni kosa la kisheria," alisema Prof Lema.

Pia alisema wahandisi wazawa wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi za kusimamia na kutekeleza miradi na kwamba wapo wanaotekeleza miradi ya kimataifa hivyo akawataka wale ambao hawajasajiliwa wajitokeze na wasajiliwe.

Makamu Mkuu wa MUST, Prof. Aloyce Mvuma, alisema mhadhara huo ulikuwa mfululizo wa matukio ya chuo kuelekea mahafali ya tisa yanayotarajiwa kufanyika leo.

# Mkuu UDOM asisitiza vijana uzalendo

**Na Waandishi Wetu**

MKUU wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Dk. Stargomena Tax, amewataka vijana kuwa wazalendo, akisisitiza kuwa mataifa huangukia kwenye machafuko yanayochangiwa na kukosekana kwa uzalendo.

Dk. Stargomena ambaye pia ni Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alitoa rai hiyo jana jijini Dodoma wakati wa mahafali ya 12 ya chuo hicho ambayo yalikwenda sambamba na kumsimika Mkuu wa Chuo hicho baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kumteua Juni mwaka huu.

Akizungumza katika mahafali hayo, Dk. Stargomena aliwaeleza vijana kuwa hawana budi kuwa wazalendo kwenye nchi yao.

"Uzalendo ni kuipenda nchi yako, kulipenda taifa lako kwa moyo wako wote na kulitetea wakati wote na sehemu yoyote uliopo, mataifa huanguka katika machafuko na miongoni mwa sababu ni kukosekana kwa uzalendo. "Mmemaliza maisha ya shule kama ilivyoelezwa, sasa mnakwenda kuanza maisha mapya. Ni rai yangu, hata pale mtakapokumbana na matatizo yasiwafanye kuacha uzalendo wenu, bali yazidi kuwaimarisha na kuwaongezea ubunifu na uthubutu," alisema.

Aliwakumbusha kuwa taifa linategemea zaidi vijana katika nyanja zote za jamii na uchumi.

"Vijana ni sikio, jicho na mlinzi wa taifa lolote duniani, amani na usalama wa nchi unawategemea ninyi ninatoa wito huu kama Mkuu wa Chuo lakini pia kama Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa," alisema.

Pia aliwaeleza wahitimu kuwa siyo kila matatizo kwenye jamii yanahitaji fedha, akifafanua kuwa yapo yanayohitaji mawazo, ubunifu, kujituma, uzalendo na uthubutu.

"Kusoma na kuhitimu ni fursa kwani siyo Watanzania wote waliobahatika kufikia hatua hii, tumieni elimu mliyopata kwa maarifa na busara ili iwe na manufaa kwenu binafsi, familia zenu na kwa taifa," alisema.

Aliwataka viongozi na wanafunzi wanaoendelea na masomo kuitunza miundombinu iliyopo ili idumu muda mrefu na kunufaisha vizazi vijavyo.

Dk. Stargomena pia alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumwamini na kumteua kuwa Mkuu wa Chuo hicho.

"Hii ni imani kubwa na kama mkuu wa chuo nitafanya kazi kwa bidii na maarifa katika kuhakikisha chuo kinafikia malengo yake kwa kushirikiana na baraza la chuo na watumishi wote," alisema. Aliomba ushirikiano ili kuhakikisha malengo ya chuo yanafikiwa na kutaka matatizo yanapotokea wajitahidi kuyabadilisha kuwa fursa na kuzitatua kwa maarifa, weledi na ushirikiano.

"Uimara na mafanikio ya chuo ni muhimu kwa mustakabali wa chuo na kuanguka kwa chuo ni anguko letu sote hususani sisi viongozi na wanachuo. Tangu kuanzishwa kwa chuo mwaka 2007 kimekuwa na maendeleo makubwa, ni jambo la kujivunia, hatuna budi kuendeleza zaidi," alisema. Mwenyekti wa Baraza la Chuo hicho, Gaudensia Kabaka, alisema chuo kimepitisha mpango mkakati wa kuanzia mwaka 2021/22 hadi 2025/26 ambao una malengo 10.

Aliyataja malengo hayo kuwa ni pamoja na kuwa chuo bora Tanzania ifikapo mwaka 2026 na kuwa miongoni mwa vyuo 20 bora Afrika ifikapo mwaka 2030.



Machinga na mizigo yao wakirejea eneo waliloondolewa eneo la Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam jana, ili kupanga bidhaa zao, ingawa wametakiwa kwenda katika masoko waliyotengewa. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Jumuiya Kiislamu yahamasisha watu kupata chanjo ya corona

**Na Faustine Feliciane**

JUMUIYA ya Waislamu ya Madhehebu ya Ahmadiyya imesema inaunga mkono juhudi za serikali kuhamasisha wananchi kupata chanjo ya UVIKO- 19 inayoendelea kutolewa maeneo mbalimbali nchini.

Akizungumza wakati wa kufunga kongamano la kitaifa la kila mwaka la wanaume wa madhehebu hayo wenye umri kuanzia miaka 40, Mwenyekiti (Sadr Majlis) wa taasisi ndogo ya wanaume wenye umri huo wa dhehebu hilo (Majlis Ansarullah Ahmadiyya), Ally Hamis Mbambwa, alisema dini yao inakubaliana na hali hatua zinazochukuliwa na serikali kutokana na hali halisi iliyopo sasa duniani ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19.

Alisema wanaunga mkono juhudi za serikali kutoa chanjo kwa wananchi wake na wao wanawahimiza waumini wao kupata chanjo kujikinga na ugonjwa huo.

Kiongozi huyo alisema hakuna namna wa Ahmadiyya wanaweza kujitenga na hali inayoendelea sasa duniani kote, hivyo wana wajibu wa kuelimisha na kuwashauri waumini wao kufuata maelekezo yanayotolewa na serikali kupitia mamlaka zake kujikinga na UVIKO-19.

"Hapa tumekutana zaidi ya wanaume 200 wa umri kuanzia miaka 40 na kuendelea na katika mambo yetu tunayofundisha hapa ni pamoja na kuwataka kuchukua hatua zote za kujikinga na huu ugonjwa ikiwa ni pamoja na kuchanja na hapa asilimia kubwa wamepata chanjo.

"Dini yetu inafuata misingi sahihi ya Uislamu ikiwa ni pamoja na kufuata taratibu na sheria za nchi," alisema Mbambwa.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmaddiya, Seif Nakuchima, alisem jumuiya yao ina ushirikiano mzuri na viongozi wa dini zingine linapokuja suala lenye mslahi mapana ya taifa na wananchi wake.

"Tumekutana hapa sisi wanaume watu wazima, lakini pia ipo mikutano mengine kama hii maalumu kwa ajili ya vijana na wanawake na wao wanapeana elimu wanayostahili lakini pia mambo kama haya ya UVIKO-19, wanapewa elimu na kuhamasishwa kwenda kupata chanjo," alisema.

Kongamano hilo la wanaume wa Ahamaddiya limefanyika kwa siku tatu kwenye viwanja vyao vilivyopo Msongola Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam.

# Abu Dhabi yaiahidi misaada Tanzania

**Na Benny Mwaipaja,** ABU DHABI

ABU Dhabi imeahidi kuendeleza ushirikiano katika masuala ya kiuchumi na kijamii na Tanzania ili kuwaletea wananchi wake maendeleo.

Ahadi hiyo ilitolewa mjini Abu Dhabi, Falme za Nchi za Kiarabu na Naibu Waziri Mkuu ambaye pia ni Waziri anayeshughulikia masuala ya Rais, Sheikh Mansour bin Zayed Al Nanyan, baada ya kupokea ujumbe maalumu kutoka kwa Rais Rais Samia Suluhu Hassan, uliowasilishwa kwake na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Ikulu ya nchi hiyo.

Akizungumza baada ya mazungumzo yao ya faragha, Waziri Nchemba alisema kuwa Sheikh Mansour ameahidi kutuma ujumbe maalumu nchini kwa ajili ya kuangalia miradi mbalimbali ya kimkakati inayotekelezwa hivi sasa na mingine mipya kwa ajili ya kutoa fedha.

Dk. Nchemba aliitaja miradi iliyowasilishwa kwa Serikali ya Abu Dhabi ni ile ya uendelezaji wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), mradi wa Ujenzi wa Bwala la Kuzalisha Nishati ya Umeme wa Mwalimu Julius Nyerere, ujenzi wa miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, kilimo na uvuvi pamoja na elimu.

"Kwenye sekta ya elimu tumejenga madarasa mengi, tumejenga vituo vya afya vingi sana na vingine viko vijijini, lakini hatujajenga nyumba za watoa huduma wanaotakiwa kufanyakazi kwenye maeneo hayo," alisema Dk. Nchemba.

Aidha, alisema wamejadiliana na Sheikh Mansour bin Zayed Al Nanyan kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo nchini zinazotokana na Tanzania kuwa lango la kibiashara kwa nchi zisizozungukwa na bahari ambazo zikitumiwa vizuri kama vile uwapo wa nishati ya mafuta na gesi, zitaifanya nchi ipae zaidi kiuchumi.

"Maeneo mengine tuliyojadiliana ni namna ya kutumia na kuishirikisha sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kuleta faida kwa pande zote mbili na wananchi kwa ujumla," aliongeza Nchemba.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi-Ofisi ya Rais-Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Jamal Kassim Ali, alisema mkutano wao na Naibu Waziri Mkuu wa Abu Dhabi uliangazia pia masuala ya Zanzibar ambapo miradi kadhaa ya kimkakati inayotaka ufadhili iliwasilishwa.

Aliitaja miradi hiyo ni ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Manga Pwani kwa njia ya ubia kati ya Serikali na Sekta Binafsi, ujenzi wa nyumba za makazi za gharama nafuu zipatazo 10,000 kwa ajili ya watumishi wa umma pamoja na wananchi wengine na uchimbaji wa mafuta na gesi.

Aliishukuru Abu Dhabi kwa kuendeleza ushirikiano na Tanzania hususan Visiwa vya Unguja na Pemba ambapo nchi hiyo ya Kiarabu ilifadhili ujenzi wa Hospitali ya Wete-Pemba na kwa kuahidi kuwa tayari kuendeleza ushirikiano huo katika miradi mipya iliyowasilishwa kwao.




Meneja Mauzo wa Tigo Arusha, Salim Shangweli (kulia), akifafanua jambo KWA Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Said Mtanda (wa pili kulia), alipitembelea banda la Tigo katika maonesho ya biashara Arusha (Arusha Trade Fair), katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki yajitosa kukabili uhaba ajira kwa vijana

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

KATIKA kukabiliana na tatizo la uhaba wa ajira kwa vijana nchini, Benki ya Ushirika ya Kilimanjaro (KCBL) imezindua mradi wa mikopo ya bajaji ili kuwakwamua kiuchumi.

Akizindua huduma ya mikopo hiyo katika viwanja vya soko la Manyema jana, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Moshi, Juma Rahibu, alipongeza hatua hiyo na kudai kuwa itaongeza fursa za ajira kwa vijana.

"Niipongeze benki ya KCBL kwa hatua hiyo kwa kuwa kubuni na kuanzisha mikopo hii kutaongeza kasi ya maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na jamii kwa ujumla kwa kuwawezesha wananchi kupunguza umaskini na kuongeza uwezo wa kujitegemea wenyewe," alisema.

Meya alisema hatua hiyo itasaidia serikali katika kuwawezesha wananchi wa kipato cha chini kujikwamua na kuiomba benki hiyo kuendeleza jitihada hizo kwa makundi mengine maalumu ya wanawake na walemavu.

"Niwaombe sana benki hii msiishie hapa kwa vijana bali huu uwe ni mwanzo wenye uendelevu kwa kubuni bidhaa zaidi za mikopo kwa wanawake na watu wenye ulemavu ili tuunge mkono juhudi za serikali katika kupambana na umaskini," alisema. Meneja Mkuu wa KCBL, Godfrey Ngura, alisema wataendelea kuhakikisha wanatoa huduma zenye malengo ya kugusa maisha ya watu kwa kuwawezesha kutoka kwenye hatua moja kwenda hatua bora zaidi kiuchumi.

Alisema dhamira ya benki hiyo ni kuona wananchi wengi wanapata huduma za kifedha kupitia benki zenye tija zitakazoendelea kubadili maisha ya wananchi wengi.

"KCBL inafanya kazi ili kufikia lengo la kuona kila mwananchi anapata fursa ya kutumia mifumo rasmi ya kifedha, hivyo huduma hii ya mikopo ya bajaj ni njia ya kuongeza mtaji na kuwafikia wananchi wengi zaidi," alisema. Meneja alisema KCBL imekopesha bajaj mpya 22 zenye thamani ya Sh. millioni 140 kwa vijana wa Manispaa ya Moshi kwa lengo la kuwawezesha kuendelea kujiajiri kupitia biashara hiyo ya usafiri.

"Mpango huu utafanywa kwa awamu ya pili na ni mpango endelevu katika kuendeleza na kupanua fursa za ajira kwa vijana," alisema.

Katibu wa Waendesha Bajaj na Bodaboda, Rashid Omari, aliwataka vijana hao kuhakikisha wanatumia na kutunza vyema bajaj hizo ili zidumu kwa muda mrefu na kuwasaidia kujikwamua kiuchumi.

# WB kupendezesha h/shauri 45 nchini

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BENKI ya Dunia(WB) imetenga zaidi ya kiasi cha Sh. trioni 1.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miuondombinu ya barabara, mitaro, masoko, maeneo ya viwanda na vituo vya mabasi katika halmashauri 45 zinazokuwa kasi hapa nchini.

Hata hivyo, utekelezaji wa miradi hiyo awamu ya kwanza utaanza na halmashauri 12 ikiwamo ya Manispaa ya Kahama ambayo imepata kilometa saba za barabara za mjini, kilometa 12.6 eneo la uwekezaji Zongomela na kituo cha mabasi Mbulu. Hayo yalibainishwa jana na mtaalamu kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI kitengo cha miradi inayotekelezwa kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Mhandisi Rashidi Mtamila, wakati akitoa taarifa ya miradi itakayotekelezwa chini ya mpango wa uboreshaji wa miundombinu katika miji ya Tanzania (TACTIC) iliyofanyika katika wilayani Kahama, mkoani Shinyanga.

Alisema, Benki ya Dunia imetenga kiasi cha dola za Kimarekani milioni 500 sawa na zaidi ya Sh. trioni 1.5 kwa ajili ya utekelezaji wa miundombinu ya barabara, masoko, maeneo ya viwanda na vituo vya mabasi katika halmashauri 45 nchini. Alisema, utekelezaji wa miradi ya namna hiyo imetekelezwa mikoa ya Mtwara, Tanga, Iringa, Sumbawanga, Mwanza, Arusha, Mpanda na Dodoma na mradi utakaapoanza Julai mwaka 2022, viongozi wa maeneo husika, madiwani na wananchi wataombwa kushiriki moja kwa moja.

"Halmashauri ya Manispaa ya Kahama ni mojawapo iliyopata miradi mingi katika fedha hizi huku halmashauri ya jiji la Mbeya ikiongoza kwa miradi hii kutokana na kukidhi baadhi ya vigezo vilivyokuwa vimewekwa ikiwamo idadi kubwa ya wingi wa watu," alisema Mhandisi Rashidi.

Naye Ofisa kutoka Ofisi ya Rais TAMISEMI, Beatrice Mchome, alisema barabara zote zitakazojengwa zitakuwa na kiwango bora cha lami ikiambatana na miundombinu ya mitaro mikubwa ya kupitishia maji na taa za kisasa ili kuimarisha usalama wa watumiaji wakati wote. Alisema katika ujenzi huo watawashirikisha wadau wa Mamlaka za Maji, Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mazingira na Jeshi la Polisi Kitengo ya Usalama Barabarani ili kutambua maeneo korofi na kuepusha migogoro inayoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa miradi.

Kwa upande wake, Mkuu wa wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, aliwataka Madiwani wa Manispaa ya Kahama kutoa ushirikiano na wasiwe sehemu ya kikwazo cha utekelezaji wa miradi hiyo.

Pia alisema, fedha hizo ni matunda ya safari za Rais Samia Suluhu Hassan nchi za nje kushawishi wawekezaji na kutangaza fursa zilizopo hapa nchini na kuwaomba Maofisa wa Benki ya Dunia kuja kuwekeza wilayani hapo kwa sababu maeneo ya uwekezaji yapo mengi.

## Rasilimali fedha kikwazo kuingia kilimo cha kisasa

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema uhaba wa rasilimali fedha ni kati ya vikwazo kuingia kwenye kilimo cha kisasa chenye tija na kuongeza pato la taifa.

Waziri wa Kilimo, Prof Adolf Mkenda, aliyasema hayo jijini Dar es Salaam wakati akizindua huduma ya utoaji dhamana ya mikopo ya kilimobiashara kidigitali, inayowezeshwa na taasisi ya PASS Trust.

Alisema sekta ya kilimo imeajiri kwa asilimia 60 Watanzania ambao hufanya shughuli zinazohusiana kisekta, ingawa bado hawajanufaika, walionufaika ni wachache ikilinganishwa na umuhimu wake.

"Kilimo ni muhimu na tunakitegemea kwa asilimia 100. Usalama wa nchi ni chakula pamoja na kuwapo majeshi. Tunahitaji fedha ili kilimo kiingie kwenye mfumo wa umwagiliaji badala ya kutegemea mvua pekee kwa sababu kuna mabadiliko ya tabianchi duniani kwa sasa na mvua hazitabiriki," alisema Prof. Mkenda.

Alibainisha kwamba mapinduzi ya kilimo yatachangiwa na matumizi ya TEHAMA, uhakika wa pembejeo za kilimo na huduma za ugani ili kuongeza ufanisi na uzalishaji kwenye sekta hiyo.

Mkurugenzi wa PASS Trust, Yohane Kaduma, alisema taasisi hiyo inawawezesha wakulima kupata mikopo katika taasisi za fedha kupitia udhamini wa kati ya asilimia 20 hadi 60, huku wanawake na vijana wakipewa kipaumbele kwa kupata udhamini hadi asilimia 80.

"Hii ni kwa wafanyabiashara za kilimo ambao wanapata changamoto za kukopa kwenye benki kutokana na kukosa dhamana ya kutosha. Tunawasaidia wafanyabiashara wa kilimo katika kuandaa mipango ya biashara ambayo anauza ili kupata mikopo katika benki," alisema Kaduma.

Kaduma alisema kufikia Septemba mwaka huu, taasisi imewawezesha Watanzania million 2.5 kupitia udhamini wa miradi 52,440 yenye thamani ya shilingi trilioni 1.24 kwa dhamana ya shilingi bilioni 565.4.

"Asilimia 47 ya wanufaika hawa ni wakinamama. Kupitia udhamini huu, PASS imeweza kutengeneza ajira zipatazo milioni 2.6. Dhamana za mikopo kidigitali inachochea upatikanaji wa mitaji ya kilimo biashara," alisema Kaduma.

Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi kutoka benki ya CRDB, Farida Mbwana, akizungumza kwenye uzinduzi huo kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, alisema, asilimia 49 ya wanufaika wa mikopo kupitia CRDB, wametokana na dhamana za PASS.

Alisema kupitia dhamana za mikopo inayotolewa na benki hiyo, zimetolewa Sh. bilioni 162.4 mwaka huu, kwa wakulima na wadau wengine katika kukuza mnyororo wa thamani katika mazao, uvuvi, mifugo na misitu.

# Kortini madai kusafirisha dawa za kulevya

**Na Hellen Mwango**

WATU wawili wakazi wa jijini Dar es Salaam, Said Shewali na Salum Athumani, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroine.

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao juzi jioni katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Romuli Mbuya.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali, Yusuf Aboud, alidai kuwa Novemba 25, 2021 katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere washtakiwa hao kwa nyakati tofauti walitenda kosa hilo.

Imedaiwa mshtakiwa Shewali alikutwa akisafirisha kilogramu 3.85 za dawa za kulevya huku Athumani yeye alikutwa akisafirisha kilogramu 3.6 za Heroine.

Hata hivyo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote kwa kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi ambazo husikilizwa Mahakama Kuu.

Kesi hizo zimeahirishwa hadi Desemba 29,2021 kwa ajili ya kutajwa. Kwa mujibu wa upande wa mashtaka, haujakamilika.




Mwenyekiti wa Jamii ya Tamil Sangam waishio nchini Balasubramaniyan Venkadachalam (kulia) akikabidhi hati maalumu ya makabidhiano ya madawati 60 kwa Mkuu wa Shule ya Zanaki, Adolf Rwegoshora kati ya madawati 157 yaliyotolewa na jamii hiyo katika shule za Upanga, Maktaba na Lumumba zote za jijini Dar es Salaam yenye thamani ya shilingi milioni 18. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shule 4 Dar zasaidiwa madawati

**Na Sabato Kasika**

SHULE za msingi Zanaki, Upanga, Maktaba na Lumumba za jijini Dar es Salaam, zimepata msaada wa madawati 157 yenye thamani ya Sh. milioni 18, ambao umetolewa na taasisi ya Tanzania Tamil Sangam.

Msaada huo ulitolewa juzi, huku wadau wa elimu wakiombwa kusaidiana na serikali kutatua kero mbalimbali zinazozikabili shule za umma ili kukuza sekta hiyo na kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

Akizungumza kwa niaba ya walimu wa shule hizo, Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Zanaki, Adolf Rwegoshora, alisema, wadau wa elimu wamekuwa mfano mzuri wa kuigwa kutokana na mchango wao.

"Ni vyema wadau wa elimu wakaunga mkono jitihada za serikali za kutatua kero za elimu kwenye shule kama ambavyo kampuni hii inavyoboresha mazingira ya shule yetu ya Zanaki," alisema Rwegoshora.

Alifafanua kuwa yeye ndiye mwenyeji wa wafadhili hao, amefanikiwa kuwashawishi wakatoa msaada wa madawati kwa shule jirani za Upanga, Maktaba na Lumumba.

"Kampuni hiyo imeunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu, imetoa madawati 37 kwa Shule ya Msingi Upanga, mengine 30 kwa Shule ya Msingi Lumumba, Shule ya Msingi Maktaba nayo imepata madawati 30 na shule yangu imepata 60, ambapo jumla ni madawati 157," alisema.

Alisema, pamoja na jitihada zake za kushawishi wafadhili hao, bado anaomba wadau wengine wa elimu kusaidiana na serikali katika kutatua kero za elimu zinazozikabili shule mbalimbali.

Mwenyekiti wa taasisi hiyo, Balasubramaniyan Venkadachalam, alisema inaendelea kupanua shughuli zake kadri inavyowezekana ili kutatua kero katika shule za msingi na sekondari za jijini Dar es Salaam.

"Katika shule ya Msingi Zanaki tulianza mwaka jana na sasa tumesaidia shule nyingine zaidi za msingi kwa kutoa idadi hiyo ya madawati yenye thamani ya Sh. milioni 18," alisema Venkadachalam.

Venkadachalam alisema, taasisi yake pia imekuwa ikitoa msaada wa vifaa mbalimbali katika shule za msingi na sekondari ikiwamo ya Gogoni, kama njia ya kuboresha elimu nchini.

# Makamba ataka wawekezaji viwanda vya vifaa vya umeme

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amewataka wawekezaji kuendelea kujitokeza na kuwekeza katika viwanda vya kuzalisha vifaa vya umeme, ili kufanikisha lengo la serikali la kutumia bidhaa za ndani katika utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini.

Amesema kwa kufanya hivyo kutafanya kuwapo kwa upatikanaji wa umeme wa uhakika nchini, pamoja na vitongoji vyote nchini kufikiwa na umeme.

Aliyasema hayo jijini Dar es Salaam baada ya kutembelea kiwanda cha kuzalisha nyaya na vifaa vya umeme cha Africab kilichopo Kurasini jijini Dar es Salaam.

Kwenye ziara hiyo Makamba ambaye aliambatana na Naibu Waziri wa Nishati, Stephen Byabato, pamoja na mambo mengine, alisema viwanda vya namna hiyo ni muhimu na vinahitajika zaidi ili kupunguza utegemezi wa vifaa kutoka nje ya nchi. Alisema mpango wa serikali kwa sasa ni kuhakikisha Wakala wa Nishati Vijijini (REA) inasambaza umeme katika vitongoji vyote nchini na hiyo ni baada ya kufanikiwa kupeleka umeme kwenye vijiji.

"Tuna vitongoji 64,000 kati ya hivyo 27, 000 vimefikiwa na umeme, zaidi ya 30,000 bado havijafikiwa na huduma ya umeme....tumedhamiria katika kipindi cha miaka minne vitongoji hivyo lazima vifikiwe na huduma hiyo, kwa kufanikisha hilo inatupasa tuhakikishe tuna vifaa vya kutosha vyenye ubora, nimefarijika baada ya kutembelea kiwanda hiki kinafanya kazi nzuri sana," alisema Makamba.

Waziri Makamba alisema maeneo ambayo hayajafikiwa na umeme zinahitajika kilometa 122,000 za nyaya za umeme mdogo na kilometa 110,000 za nyaya kwa umeme wa kati, jumla zinahitajika kilometa 340,000 za nyaya za umeme.

Makamba alisema pia zinahitajika transfoma 38,000 ili kufikisha umeme katika vitongoji vyote nchini, watumiaji zaidi ya milioni tatu wanatarajiwa kufikiwa.

"Nimeshuhudia uzalishaji unaoendelea hapa ila bado tunahitaji kuongeza, nimefurahi kuna mpango wa kuongeza kiwanda na niwaombe wawekezaji wengine wasisite kujitokeza na kuwekeza katika sekta hii ya Nishati," alisema Makamba.

Meneja Masoko wa Africab, David Tarimo, alisema kiwanda hicho kina uwezo mkubwa wa kuzalisha vifaa na kwa kutambua ukubwa wa uhitaji wameongeza uwekezaji kwa kufungua kiwanda kingine katika eneo la Kimbiji.

"Kuna kiwanda kingine tumeanzisha kule Kimbiji ili kuongeza uzalishaji na tutaendelea kuhakikisha tunazalisha bidhaa zetu katika ubora unaohitajika sokoni pamoja na kutoa ajira kwa vijana wa kitanzania," alisema Tarimo.

Aidha, Tarimo aliishukuru Serikali kwa kuendelea kushirikiana nao na kuiomba iendelee kuweka mkazo wa matumizi ya bidhaa za ndani hasa katika kuhakikisha ubora wa utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa kuwa Tanzania kwa sasa ina uwezo na hakuna sababu ya kuruhusu bidhaa nyingi ziingie kutoka nje ya nchi

## Waziri awahimiza wafugaji kumiliki maeneo ya malisho

**Na Mbaraka Kambona,** GEITA

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki amewahimiza wafugaji kuwa na maeneo ya kulishia mifugo yao, jambo ambalo litawapunguzia migogoro inayowakumba kila uchao.

Waziri Ndaki alitoa wito huo alipokuwa akizungumza na wafugaji wa vijiji vya Luhembela na Masumbwe vilivyopo wilayani Mbogwe, mkoani Geita juzi.

"Wafugaji tukumbuke kwamba maeneo mengi tunayotumia kuchungia mifugo yetu ni maeneo huria yanayomilikiwa na Serikali, lakini ni vizuri sasa tukaanza kuwa na maeneo yetu na tuyalinde kisheria kwa kuyakatia hati ya kimila au ya kawaida," alisema.

Alisema kuwa haiwezekani mfugaji awe na ng'ombe 1,000 halafu eneo la kuchungia hana, huo ndio mwanzo wa mahangaiko na kuingia katika migogoro na watumiaji wengine wa ardhi hususan wakulima.

"Sisi Serikali tutawasaidia, maeneo hayo mtakayoyanunua yarasimisheni, yakatieni hati ili yawe ya kwenu, angalau uwe na eneo la kuanzia ili hata unapoiambia Serikali kuhusu malisho una eneo la kwako la kuanzia," alisisitiza.

Aliongeza kwa kusema kuwa endapo wafugaji wataendelea kufuga kwa kutegemea maeneo huria wataendelea kuwa katika migogoro na itafika mahala watakosa pa kuchungia na hatimaye watawauza ng'ombe wote.

Awali, mfugaji wa kijiji cha Luhembela, Maisha Magenya alimueleza Waziri Ndaki kuwa ng'ombe wanao na wanahitaji kuendelea kufuga, lakini wanakosa elimu ya namna bora ya ufugaji kwa sababu ya uhaba wa wataalamu katika wilaya yao.



Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara, Abdallah Mohamed Malela (wa pili kushoto), akijaribu ubora wa trekta lililotolewa na Benki ya NBC kwa mshindi wa droo ya sita ya kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani'ambae ni Chama Kikuu Cha Ushirika wa wakulima Mtwara-Masasi ( MAMCU) wakati wa kukabidhi zawadi hizo mkoani Mtwara. Wanaoshuhudia ni pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dastan Kyobya (wa sita kushoto), Mkurugenzi wa Fedha wa benki hiyo, Waziri Barnabas, viongozi wa wakulima na wa MAMCU. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushirika wa Mtwara wazawadiwa trekta

**Na Mwandishi Wetu,**
MTWARA

WASHINDI wa droo ya sita ya kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani'kutoka mikoa ya Mtwara na Lindi, wamekabidhiwa zawadi mbalimbali zikiwamo baiskeli, pikipiki, guta na trekta.

Zawadi hizo zimekabidhiwa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC), huku serikali ikibainisha kuwa zawadi hizo zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuchochoea kasi ya uzalishaji wa mazao ya korosho na mazao mengine katika mikoa hiyo.

Akizungumza katikati ya wiki mkoani Mtwara wakati wa kukabidhi zawadi hizo kwa washindi mbalimbali wa droo hiyo ikiwamo zawadi kubwa ya trekta kwa Chama Kikuu Cha Ushirika cha Wakulima Mtwara-Masasi ( MAMCU), Katibu Tawala Mkoa wa Mtwara, Abdallah Mohamed Malela, alisema zawadi hizo zimetolewa wakati mwafaka kwa kuwa mkoa huo upo kwenye utekelezaji wa mkakati wake wa kuongeza uzalishaji wa zao la korosho kutoka tani 280,000 zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani 700,000 ifikapo mwaka 2025.

"Zaidi pongezi nizielekeze kwa MAMCU kwa kuwa wanapokea zawadi hii ya trekta ikiwa ni hivi karibuni tu kama mkoa tuliweka azimio la msingi kwamba kuanzia msimu ujao wa kilimo kila chama kikuu cha ushirika lazima kiwe na shamba darasa lenye ukubwa wa ekari 1,500 ili kufikia malengo ya uzalishaji wa mazao ya korosho na mazao mengine ya kimkakati. Kupitia zawadi hii ni wazi NBC imewashika mkono naomba na nyinyi pia muishike mkono," alisema.

Malela aliwasisitiza wakulima mkoani humo kuhakikisha wanahifadhi fedha zao benki sambamba na kuongeza nidhamu ya matumizi ya fedha zao hata pale wanapozihifadhi kwenye taasisi za kifedha na wazitumie kwenye mahitaji ya msingi ikiwamo kuwekeza zaidi kwenye zana za kilimo cha kisasa ili kuboresha hali za maisha yao na familia zao.

Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dastan Kyobya, aliahidi kutoa eneo la ekari 1500 kwa MAMCU ili kutumika katika kufanikisha shughuli za kilimo cha ushirika huo, ikiwa ni ishara pia ya kuunga mkono nia njema ya Benki ya NBC katika kuwasaidia wakulima hao.

"Kwa kuwa NBC tayari wameanza kwa kuwazawadia zana za kilimo ikiwemo trekta na sisi serikali ya mkoa tunawapatia eneo la kutosha ekari 1500 ili muweze kufanikiwa azimo la kulima ekari 1500 katika msimu ujao wa kilimo...hongereni sana," alisema Kyobya.

Mkurugenzi wa Fedha wa NBC, Waziri Barnabas, alisema tangu kuanza kwa kampeni hiyo jumla ya washindi 139 wamejipatia zawadi mbalimbali zikiwamo baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa mikorosho, guta (Toyo) pamoja na zawadi za nyingine ikiwamo kanga, mabegi ya shule na madaftari vikiwa na thamani ya takribani Sh. milioni 200.

Nae Mkuu wa Kitengo cha Wateja Wadogo wa Benki ya NBC, Raymond Urassa, alisema kupitia droo hiyo benki ilitoa zawadi za aina mbalimbali zipatazo 26 ikiwamo trekta 1, pikipiki 7, baiskeli 9, pampu za kupulizia dawa mikorosho 8, guta (Toyo)1, pamoja na zawadi za nyingine kama kanga, mabegi ya shule na madaftari kwa wakulima mmoja mmoja, AMCOS na vyama vikuu ushirika katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

Kwa upande wao washindi wa droo hiyo waliishukuru NBC kwa kuandaa kampeni hiyo kwa kuwa imekuwa na msaada mkubwa kwao.




Ukurasa 13

Hili la vyumba vya madarasa kamwe tusilifanyie mzaha



**UWEZESHAJI WASICHANA KUPITIA KILIMO**
**Mradi wa bil. 1.6/- unaohamisha wasichana kutoka umasikini**

Ukurasa 14



# Kilimo shadidi 'kinavyowatoa' walima mpunga vijana, hadi bodaboda mtaani

• 'Haijapata kutokea' Mvomero gunia 10 hadi 45

**Na Mwandishi wetu**

VIJANA wanaojishughulisha na biashara ya kubeba abiria kwa kutumia usafiri wa pikipiki maarufu kama 'bodaboda', ambao pia ni wakulima wilayani Mvomero wameibuka na kauli wakikisifu 'Kilimo Shadidi' katika zao la mpunga, hata kuweza kubadilisha maisha yao.

Kilimo Shadidi ni msamiati kwenye kilimo cha mpunga kinachotumia maji na mbegu kidogo na kinahimiza matumizi sahihi ya mbolea, viuatilifu na kanuni nyingine za kilimo bora.

Fikiri Nestory (30) na Abdallah Makago (26) ni miongoni mwa vijana hao wanaoendesha bodaboda, kwa pamoja wanasema kabla ya wakulima kupewa mafunzo kuhusu kilimo shadidi cha mpunga, walikuwa wakivuna gunia nane hadi 10 kwenye ekari moja.

Makago anasema, ni mageuzi waliyoingia katika miaka ya karibuni kwa nguvu ya Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) kupitia mradi wake wa kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la mpunga

Ni mradi wanaoshirikiana na halmashauri ya wilaya ya Mvomero mkoano Morogoro, kwenye skimu za Mkindo na Dakawa, walitoa mafunzo mbalimbali yakiwamo ya Kilimo Shadidi, iliyowawezesha wakulima katika msimu wa mwaka 2019/20 kuongeza uzalishaji kufika wastani wa gunia 38 hadi 45 kwanye ekari moja.

Makago anasema, kabla ya kupata mafunzo hapakuwapo wastani wa gunia nane hadi 10 na hakukuwapo fursa ya biashara ya usafirishaji, kwani wakulima wengi walisafirisha mazao yao wenyewe.

Anasema ongezeko hilo la mavuno kwa wakulima waliotumia Kilimo Shadidi baada ya kupata mafunzo kutoka Baraza la Kilimo Tanzania na kuunganishwa na watoa huduma mbalimbali, wakiwamo wakala wa pembejeo na wamiliki wa zana za kilimo, imetoa fursa ya vijana kuajiriwa na watoa huduma wengine.

Kimsingi, ACT ni jukwaa la kitaifa la wadau wa sekta binafsi wanaojishughulisha na masuala ya kilimo na lengo mahususi la baraza hilo ni utetezi na ushawishi wa kuwapo mazingira wezeshi ya kibiashara kwenye sekta ya kilimo.

Mwendesha bodaboda mwingine, Richard Tadei (25), anasema 'alijiongeza' na kuchangamkia fursa ya ajira kwa vijana iliyojitokeza ya kujaza mpunga kwenye magunia kwa gharama ya sh 500 kwa gunia na kubeba (ukuli) magunia kutoka shambani hadi kwenye kituo cha kusafirishia kwa Sh 10,000 hadi 15,000 kutegemea umbali.

Vilevile, anasema kusafirisha mpunga hadi nyumbani au ghalani kumekuwa na gharama ya wastani wa Sh 5,000 hadi 10,000 kutegemea umbali, hivyo kuwa jambo la manufaa kwao.

"Biashara hii iliwavutia vijana wengi wa bodaboda, kwani kipindi hiki cha kuvuna mpunga kunakuwa na abiria wachache, kwa kuwa wengi wao wanakuwa shambani.

"Kwa siku naweza kusafirisha magunia 20 na kupata Sh. 100,000 hadi 160,000. Kwa kubeba abiria, sio rahisi kupata kiasi hicho, kama umejitahidi kubeba abiria wengi kwa siku na siku hiyo ni nzuri unaweza kupata kati ya sh 20,000 hadi 30, 000," anafafanua.



Shughuli za Kilimo Shadidi katika shamba la mpunga zikiendelea mkoani Morogoro. **PICHA: MTANDAO.**

Maelezo ya Tadei ni kwamba, msimu huo wa mavuno wa mwaka 2020/2021, amefanikiwa kusafirisha magunia ya mpunga hata imemuwezesha kununua pikipiki mpya yenye thamani ya sh milioni 2.6.

Anasema kwa upande mwingine, ongezeko hilo la uzalishaji mpunga lilifanya biashara ya mama na baba lishe kushamiri kwenye skimu za Mkindo na Dakawa, kwani kulikuwapo vibarua wengi wakiwasaidia wakulima kuvuna, kuweka mpunga kwenye magunia, kubeba mzigo (ukuli) na kusafirisha mpunga.

"Kwa kweli, mradi huu umekuwa na manufaa makubwa kwa jamii ya vijiji vya Mkindo na Dakawa hususani kwa vijana kwa kupanua wigo wa ajira. Tunashukuru Baraza la Kilimo Tanzania (ACT) kwa kuleta na kusimamia utekelezaji wa mradi huu," anasema.

Wakulima, wanasema kukosekana miundombinu hususani kwenye skimu ya Mkindo, kumefanya gharama za uzalishaji kuongezeka kwa kusafirisha gunia moja kutoka shambani hadi nyumbani au ghalani kufika kati ya Sh. 10,000 hadi 20,000.

"Gharama hizi ni kubwa sana na zinapunguza kipato cha mkulima. Tunaliomba Baraza la Kilimo Tanzania litusaidie kutatua changamoto hii," anasema.

Mratibu wa Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani Shindani na Endelevu wa zao la mpunga, Henry Mziray, anasema lengo la mradi ni kupanua wigo wa ajira na kipato kwa wanawake na vijana, ili waweze kuboresha maisha yao.

"Mradi huu unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) kupitia Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo (IFAD) na Mtandao wa Vyama vya Wakulima Kusini mwa Bara la Afrika (SACAU), una lengo la kunufaisha kaya 1,600 za wakulima wadogo na wajasiriamali wanaojishughulisha na kilimo cha zao la mpunga kwenye skimu za Dakawa na Mkindo, wilayani Mvomero," anasema.

Kimsingi, ACT ni jukwaa la kitaifa la wadau wa sekta binafsi wanaojishughulisha na masuala ya kilimo na lengo mahususi la baraza hilo ni utetezi na ushawishi wa kuwapo mazingira wezeshi ya kibiashara kwenye sekta ya kilimo.

UCHUMI

# Wanaosoma Chuo Kikuu Muhimbili wajitosa vita ukatili ngono kuokoa wenzao wasio nacho

- Wageni Dar hunasa zaidi mdomoni mwa simba
- Hafla yaja wiki hii kuchangisha pesa za kampeni
- Waupa 'tano' uongozi kudhibiti ufaulu kingono



Mwanahabari wa Nipashe (kushoto), akiwahoji viongozi wa Serikali ya Wanafunzi ya Chuo Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili. Kutoka kulia ni Esther Moses (Katibu) na Joseph Madinda (Waziri wa Jinsia na Ustawi wa Wanafunzi).

**Na Devota Mwachang'a**

SILAHA kubwa dhidi ya ukatili kijinsia, ikiwamo ukatili kingono, ni namna ya kujua mbinu za kuzuia isitokee na jukumu la kuwalinda wanawake na wasichana wasiangukie ukatili huo katika jamii wanamoishi.

Kimsingi, wasichana au wanafunzi hurubuniwa kuingia kwenye mtego wa kujipatia pesa na kujikuta wanafanyiwa ukatili kingono au unyanyaswaji kingono, kama vile kubakwa na kulazimishwa matendo yenye viashiria vya ngono.

Hivyo, serikali ya wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHASSO), imeamua kupambana kumuepusha mwanachuo na kumlinda dhidi ya ukatili huo wa kingono.

**MWANAHARAKATI MWANAUME**

Akizungumza na Nipashe, Waziri wa Jinsia na Ustawi wa Wanafunzi wa MUHASSO, Joseph Madinda, anataja changamoto kubwa inayowakabili wanafunzi ni ukosefu wa fedha, mazingira yanayowaingiza kwenye hadaa hata wakanasa kwenye mtego wa ukatili kingono.

"Tunaandaa hafla ya chakula tumeiita 'Revo-wellness' itakayofanyika tarehe 18 Desemba 2021 maeneo ya hapa chuoni, kwa lengo la kuchangisha pesa toka kwa wahisani.

"Tunaanzisha mfuko maalumu utakuwa chini ya wizara yetu, kwa ajili ya kusaidia wanafunzi ambao kutokana na kukosa pesa, wapo hatarini kujiingiza kwenye mambo yasiyofaa ili wajipatie pesa waendelee na masomo," anaeleza Madinda.

Anafafanua kwa mfano wanaosoma diploma, hawana mikopo na familia wanazotoka zinatofautiana kiuchumi, baadhi wa hali ya chini, hivyo inachangia kuwapo wanafunzi wanakosa kabisa pesa za kuendesha maisha yao chuoni.

"Angalau sisi wanaume tunapambana kukabiliana na hali ngumu ya maisha hapa chuoni, hata pale tunapokosa pesa, lakini hali ni mbaya kwa wanafunzi wa kike.

"Wao ni ngumu kuvumilia na hujikuta wanajiingiza kwenye tabia hatarishi kama umalaya kwa ajili ya kupata pesa. Wanaweza kujirahisisha kwa wanaume ndani na nje ya mazingira ya chuo," anafafanua Madinda.

Anasema jukumu lao viongozi ni kuwatengenezea wanafunzi mazingira rafiki kupata elimu bila kuingiliwa na tabia hasi zinazowaweka hatarini, ikiwamo changamoto ya kukosa ada za masomo.

"Tumealika viongozi na kampuni mbalimbali ikiwamo (benki) NMB, Vodacom na wengine kwa ajili ya ufadhili wa jambo letu," anasema Mandinda.

Anaendelea: "Fedha zitakazokusanywa wakati wa hafla, zitasaidia wanafunzi wa diploma kwa kozi za maabara, famasia, mionzi, ukunga na uuguzi, afya ya mazingira na meno, ambao tuliwatambua kupitia usajili tulioshiriki kuufanya."

MUHASSO inasema imejipanga kuhakikisha usalama wa wanafunzi dhidi ya ukatili wa kingono, kwa kuandaa na kusambaza matangazo yanayowatahadharisha na kuwaelekeza wanafunzi (hasa wapya) wanapaswa kutoa taarifa iwapo watakutana na ukatili dhidi yao.

Madinda anaeleza mikakati yao, ni kutambua changamoto zinazowakabili wanachuo kwa kuwabaini walio wapya, hasa watokao nje ya Dar es Salam, ambao wamo wasio na ndugu jirani.

Anasema wanachuo hao hupokewa na wanaojifanya wasamaria wema, ili kuwafadhili makazi kipindi wakisubiri usajili, wengi wao hutekeleza ukatili kwa wanafunzi wa kike, hivyo matangazo wanayotoa MUHASSO pia yanatuma ujumbe kwa watekelezaji ukatili wa kingono.

"Jukumu letu ni kuwaambia wanafunzi wote wapya na wanaoendelea na masomo kwamba ukatili wa kingono hauvumiliki kwa hali yoyote ile," anatamka na kufafanua:

"Hivyo, tumejikita zaidi kuwapatia uelewa juu ya ukatili wa kijinsia na hasa ukatili wa kingono. Wanafunzi wanapaswa kujiamini na kutoa taarifa dhidi ya ukatili unaotendeka hapa chuoni."

Madinda ambaye ni nwanafunzi wa mwaka wa pili chuoni hapo, anaeleza kwa muda aliokuwapo masomoni, ofisi yake haijawahi kuthibitisha malalamiko au taarifa zilizofikishwa na waathirika wa ukatili wa ngono.

Anasema, hali hiyo bado haijawaondolea nia yao kuja na mbinu ya tahadhari kwa wanafunzi wa kike kuwalinda kabla hawajaingia mtegoni.

Kuhusu rushwa ya ngono, Madinda anaeleza chuoni kwao hakuna anayepewa ufaulu maksi za juu kwenye mitihani kwa rushwa, akiusifu uongozi kuwa makini kuhakikisha kila anayepata matokeo ni zao la bidii na kujituma masomoni.

Katibu wa MUHASSO, Esther Moses, anasema kukosa pesa kwa wanafunzi wa hali ya chini imekuwa changamoto inayobeba zingine na inachangia kuharibu taaluma, tabia na mienendo ya wanafunzi, hata kuwasababaishia kufanya vibaya kwenye mitihani mingi.

Esther anatoa mfano, katika muhula wa masomo uliopita walioshindwa kuendelea na masomo ni waliotumia muda wa vipindi vya darasani kufanya biashara.

"Tumefuatilia na kubaini wanafunzi wanafanya biashara nyingi. Muda wa masomo, wao wanakimbizana Kariakoo kutuma na kuchukua bidhaa. Wanajiingiza kwenye kufanya biashara na kuharibu ratiba zao za masomo.

"Wapo pia ambao hutumia muda wa masomo kwa kuwasuka wenzao nywele, ili wapate pesa, hawafanyi hivyo kwa lengo la kujiandalia maisha watakapohitimu masomo, bali kupata pesa za kuendelea kumudu maisha ya chuoni," anaeleza.

"Tunaamini kupitia matangazo yetu ya tahadhari, wanafunzi watakuwa katika mazingira salama kujua sehemu sahihi ya kutoa taarifa iwapo watakutana na kadhia ya ukatili wa kingono, ikiwamo kuja ofisini kwetu," anaeleza katibu huyo.

**NENO LA TAMWA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), Dk. Rose Reuben, anasema wamekuwa wakipambana kukabili ukatili wa jinsia miongoni mwa jamii, familia, shuleni na vyuoni.

"Jambo kubwa tunalosisitiza ni kwamba, wanafunzi wenyewe wasikae kimya kuhusiana na suala zima la ukatili wa kingono wazungumze, wasikae kimya na kufanya siri," anasema.

Dk. Reuben anafafanua kwamba iwapo wanaofanyiwa ukatili kingono wakizungumza inaibua mijadala na mbinu za kutatua jambo jipya,

Historia inaeleza kuwa TAMWA imekuwa ikipambana dhidi ya ukatili wa kingono unaoambatana na kashfa za rushwa kwenye vyuo vikuu.

Mwaka 1992 TAMWA iliibua mkasa uliomhusisha mwanafunzi wa kike wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) katika mkasa uliodhuru uhai wake.

Mnamo Desemba 7 mwaka huu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Joyce Ndalichako, alikuwa mgeni rasmi katika Siku ya Afya ya Akili, iliyofanyika UDSM, ambako alitoa angalizo dhidi ya uonevu huo.

Prof. Ndalichako anawataka wanafunzi wa kike katika taasisi za elimu kila wanapokutana na kadhia ya rushwa ya ngono, wasikubali kuingia mtegoni, bali watoe taarifa kwa idara na vitengo husika.

Msingi Mkuu wa Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya Mwaka 1998 na marekebisho yaliyofanyika 2002, imeingiza vifungu vya makosa ya kujamiiana kwenye kanuni za adhabu, kwa yeyote anayepatikana na hatia, ikiwa na adhabu ya kifungo si chini ya miaka 30 jela hadi maisha.




Tangazo lililoandaliwa na kusambazwa na MUHASSO kwenye makundi ya mitandao ya kijamii ya wanafunzi, kubandikwa kwenye ubao wa matangazo na maeneo tofauti chuoni. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Hili la vyumba vya madarasa kamwe tusilifanyie mzaha






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

MIEZI kadhaa iliyopita Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, aliagiza wakuu wa mikoa na wilaya kuhakikisha madarasa 12,000 ya sekondari na 3,000 ya shule shikizi yanakamilika kabla ya Desemba 15 mwaka huu, ili wanafunzi watakaoanza masomo Januari wasikose madarasa wala viti vya kukalia.

Ummy alitoa agizo hilo akitangaza mgawanyo wa mgawo wa fedha Sh. bilioni 535.6 kati ya Sh trilioni 1.3 ambazo serikali imepokea kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kupambana na athari za Uviko-19.

Alisema Ofisi ya Rais -TAMISEMI imeidhinishiwa kupokea jumla ya Sh. bilioni 535.68 kati ya fedha zote zilizotolewa kwenye mkopo huo wa masharti nafuu, ambayo ni sawa na asilimia 41.1.

Ummy anasema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 304 ni kwa ajili ya elimu msingi, Sh. bilioni 226.68 ni kwa ajili ya afya ya msingi na Sh. bilioni tano ni kwa ajili ya kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara wadogo.

Hivyo, kinachoendelea sasa katika halmashauri nyingi ni ujenzi wa madarasa, ili wanafunzi wa kidato cha kwanza na darasa la kwanza wasikose mahali pa kusomea, huku shule zikitarajiwa kufunguliwa mnamo Januari 17 mwakani.

Kimsingi, ujenzi wa idadi ya vyumba vya madarasa haya unatokana na mahitaji kulingana na idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Ukamilishaji madarasa 12,000 utawezesha wanafunzi 600,000 kupata vyumba vya kusomea na utaondoa changamoto ya upungufu wa vyumba vya madarasa, kwa asilimia 100 katika sekondari. Kiasi cha wanafunzi 1,022,936 wanakadiriwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka ujao.

Uamuzi huo wa serikali katika kushughulikia ujenzi wa madarasa mapema kabla ya shule kufunguliwa kama ambavyo imekuwa ikitokea miaka ya nyuma, shule zinafunguliwa ndipo ujenzi wa vyumba vya madarasa unaanza, ni hatua mwafaka.

Pamoja na shauku ya kutaka kuingia kidato cha kwanza wanayokuwa nayo wengi wao, hata hivyo hujikuta wakichelewa kuanza masomo kwa wakati, kutokana na uhaba wa vyumba vya madarasa kama ambavyo tumeshuhudia miaka ya nyuma, hivyo kusota kwa muda wakisubiri ujenzi unaoendelea ukamilike.

Hali hiyo, imekuwa ikiwafanya viongozi wa kitaifa kuingilia kati kwa kutafuta njia za dharura, huku wakitoa matamko ya kuwataka viongozi wa chini yao hususan wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi kusimamia ujenzi wa vyumba vya madarasa, katika shule ambako kuna upungufu huo.

Aidha, pamoja na pongezi kwa serikali, naomba nitoe wito wa kuwaomba viongozi wanaosimamia mchakato wa ujenzi huo, kwamba wahakikishe madarasa yanayojengwa yanakidhi viwango vinavyotakiwa.

Hakuna sababu ya kukimbilia kumaliza ujenzi wa madarasa bila kuzingatia ubora. Wasimamizi wa ujenzi huo wasikimbilie kumaliza ili kwenda sawa na agizo la Waziri.

Kujenga vyumba vya madarasa kwa mtindo wa 'zima moto' ni wazi vyumba vya madarasa havitakuwa bora na itachukua muda mfupi vitaanza kupata nyufa.

Kimsingi hilo si jambo la dharura, kazi hiyo ifanyike kwa umakini ili vyumba viwe na ubora ambavyo vitadumu kwa miaka mingi. Pia, Waziri Ummy awape nafasi wakuu wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri, ili kusimamia ujenzi huo kwa umakini. Tukifanya mzaha, mh! Alamsiki!

UCHUMI

UWEZESHAJI WASICHANA KUPITIA KILIMO

# Mradi wa bil. 1.6/- unaohamisha wasichana kutoka umasikini wa shambani hadi utajiri

• Msichana Initiative yapewa 'koleo' la mradi

**Na Elizabeth Zaya**



Kinamama wakiwajibika katika majukumu ya uzalishaji shambani. **PICHA ZOTE: MTANADAO.**

UKATILI wa kijinsia ni miongoni mwa changamoto kubwa ambazo zimekuwa zikiwakumba wanawake na wasichana wengi nchini.

Kwa mujibu wa takwimu ambazo zimekuwa zikitolewa na taasisi mbalimbali, karibu asilimia 40 ya wanawake wamepitia vitendo hivyo vya ukatili wa kijinsia kwa namna mbalimbali.

Asilimia 44 ya wanawake walioolewa, pia wanatajwa waliwahi kupitia vitendo hivyo vya ukatili kutoka kwa waume zao.

Wanawake, pia ni miongoni mwa kundi linaloishi katika lindi la umasikini kutokana na wengi kuishi kwa utegemezi kutoka kwa waume zao.

Kilimo ni miongoni mwa sekta zinazojulikana kuajiri idadi kubwa ya Watanzania hata hivyo, bado ikichimbwa kwa kina eneo hilo la wanawake linaonekana kuwekwa nyuma, nafasi ya haki zao huchukuliwa na wanaume.

Sasa kuna makundi ya kijamii yamejikita katika kupambana dhidi ya kasoro hizo, ikiwamo asasi isiyo ya kiserikali ya Msichana Initiative, inayopambana kumsaidia mtoto wa kike kupunguziwa mzigo na changamoto zinazomkwamisha katika kutimiza malengo yake kwenye nyanja mbalimbali.

Hapo mojawapo inachokifanya, ni kumuonyesha njia ya kujitafutia kipato ili aondokane na umasikini na unyanyapaa anaokutana nao. Katika kufanikisha hilo, Msichana Initiative, imekuwa inaendesha programu mbalimbali na kumwezesha binti kujikomboa kiuchumi kupitia kilimo.

**MRADI MPYA**

Taasisi hiyo kwa kushirikiana na taasisi ya Sustainable Agriculture Tanzania (SAT) na PPIZ hivi karibuni ilizindua mradi unaokusudia uwezeshaji wa wasichana wadogo kupitia kilimo, ikilenga kusaidia kupunguza vyanzo vya ukatili kwa wasichana hao, pamoja na wanawake.

Mradi huo unajulikana kwa jina 'Uwezeshaji Wasichana Kupitia Kilimo (GAPE)', ambao ni wa miaka miwili na unagharimu zaidi ya Sh.bilioni 1.6, ukitekelezwa katika mikoa ya Dodoma, Tabora na Zanzibar kwa ufadhili wa ubalozi wa Ufaransa.

Rebeca Gyumi, ni Mkurugenzi Mtendaji wa Msichana Initiative, anayesema kwamba mradi huo uko mbioni kukamilika na mpaka mwisho utakuwa umenufaisha wasichana 1000 waliochaguliwa katika mikoa miwili ya Dodoma na Tabora na wengine idadi kama hiyo kutoka Zanzibar.

Anasema kwamba lengo kubwa ni kuwajengea uwezo wasichana wenye umri wa miaka 15 hadi 24 walioko nje ya shule, ili kuwasaidia kubuni na kutekeleza miradi midogo waliyo nayo katika biashara na kilimo. Anataja miongoni mwa maeneo ambayo vitendo vya ukatili kwa wanawake vimekuwa vikifanyika, ni pamoja na katika sekta ya kilimo na kwamba tayari wameshajikita kutoa elimu kwa kundi la wasichana, katika namna ya kukabiliana au kupambana navyo wakati wakikitumia kilimo chao kujikwamua kiuchumi.

Rebeca anasema, tayari wameshawapatia semina mbalimbali wasichana katika mikoa tofauti, ikiwamo Dodoma namna ya kuendesha shughuli za kilimo bora na chenye ubunifu, kinachodumu na kuleta matunda kwao, pia kusaidia familia zao.

"Tunafahamu namna ambavyo wanawake wamekuwa wakinyanyasika kwenye sekta hii ambayo ilizoeleka kuwa ni ya wanaume pekee, lakini sisi tumejitoa kuwapa elimu hii ili kuvunja mwiko huu kwenye jamii.

"Tunataka kupitia kilimo hiki kisaidie kupunguza vitendo hivyo vya ukatili, kwa sababu wasichana na wanawake watakuwa wanachangia kipato kwenye familia zao," anasema Rebeca.

Anaendelea:"Tunaamini kwamba, kutengeneza mazingira mazuri kwa wanawake na wasichana kuendesha shughuli zao kwa uhuru bila kukumbana na vitendo hivyo vya ukatili, itawaongezea ujasiri wa kufanya kazi zaidi, pia itasaidia jamii kuamini kwamba kazi hiyo si ya wanaume peke yao. "

Kwa mujibu wa bosi huyo, ni matarajio ya programu hiyo kubadilisha mtazamo kwenye familia na jamii, kuwasaidia wanawake na wasichana wasifanyiwe ukatili kwa kuwaelimisha , baada ya kuona mchango wao na umuhimu wao kutokanana na kipato wanachokipata kupitia shughuli za kilimo.

"Kwa miaka mingi wanawake na wasichana walikuwa wakionekana kama 'magolikipa', kwa hiyo programu hii inalenga kujenga uelewa kwa jamii ya Watanzania, nafasi ya kundi hilo kwenye familia, jamii na mchango wao kwa uchumi wa nchi kwa ujumla," anasema Rebeca.

Pia, anaeleza haja ya kuwa na nafasi sawa kwa jinsia zote kushiriki katika kilimo hai na haja ya jamii kuachana na mila na tamaduni zinazodai baadhi ya mazao yanaweza kulimwa na wanaume pekee na si wanawake.

"Hakuna mazao ya kulimwa na wanaume pekee wala ya wanawake pekee, wala hakuna kazi ya kundi fulani tu, makundi yote ya jinsia zote yanaweza kulima mazao yote na kufanya shughuli zote kulingana na hali inavyoruhusu kikubwa ni kujituma na kufuata kanuni za kila sekta husika.

"Ifike wakati wanaume nao waone umuhimu kwamba wanawake nao wanamchango wao katika kuchangia pato kwenye familia, jamii na kwa taifa kutokana na kazi za mikono yao.

"Na hili ni muhimu sana kwa sababu asilimia kubwa ya waangalizi na wasimamizi wa kaya huwa ni wanawake na wako tayari kuwajibika zaidi kwa ustawi wa familia zao kuliko wanaume."

Anasema, ni muhimu kutambua mchango wa wanawake na wasichana kwenye uchumi unaotokana na kilimo, kwa sababu, mapato yanayotokana na mazao yanayouzwa na wanawake hutumika kwa manufaa ya kaya zao.

"Wanaume huwa na tabia ya kutumia pesa zao kwa masuala mengine ikiwamo mambo ambayo hayanufaishi kaya zao, ikiwamo unywaji pombe, lakini kwa wanawake si wa namna hiyo,

"Ndio maana tumeliona hilo kama Msichana Initiative, tukaona tuanze kutoa elimu kupitia mradi huu wa GAPE, kwa lengo la kuwakomboa wanawake kuwaingiza katika sekta hii ya kilimo, wajikomboe kiuchumi wao pamoja na familia zao," anasema, akiutaja ndio mwarobaini wa kupambana na kupunguza kama siyo kumaliza kabisa ukatili ambao wamekuwa wakifanyiwa."

Rebeca anaeleza kwamba wameanza kuvunja imani potofu iliyojengeka ndani katika jamii, kwamba mwanamke hawezi kuingia kwenye sekta ya kilimo na nyinginezo zinazoaminika kwamba ni za wanaume pekee yao, akisisitiza wanachokijenga kitachangia kubadili mtazamo huo na kuleta mapinduzi mapya.





## Dawa ajira kwa vijana yatajwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema ufugaji wa kibiashara ni jawabu la ukosefu wa ajira kwa vijana nchini.

Ulega aliyasema hayo jana wilayani Kongwa mkoani Dodoma, alipokuwa akizungumza na viongozi wa Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Taasisi ya PASS Trust baada ya kutembelea Kituo cha Taliri Kongwa na Kituo atamizi cha kilimobiashara kwa vijana cha PASS-AIC.

Alisema ufugaji na uvuvi wa kibiashara na kisasa ni suluhisho kubwa katika ajira kwa vijana.

"Pia itasaidia nchi katika kuongeza kipato lakini vile vile kuwasaidia watu kuondokana na hali duni, kwa hiyo kazi tunayoifanya hapa ya uatamizi ni kutengeneza wafanyabiashara wa mifugo wa kisasa."

"Tunanenepesha mbuzi ambao wanaingia sokoni na kazi hii tumeianza hapa Kongwa na tunatamani iende sehemu nyingi sana na wengine tunawakaribisha waje wajifunze hapa Halmashauri zitakazopendezwa na mradi huu waingize kwenye maeneo yao ili kutoa ajira zaidi kwa vijana wetu,"alisema.

Alisema serikali itawasaidia kupata maeneo vijana watakaovutiwa na kazi hiyo.

"Serikali kwa sasa tutawapa ardhi wale wanaokwenda kufuga na si kuchunga, pia serikali yetu imefungua milango ya kibiashara tuna viwanda viwili vikubwa vya nyama na mahitaji ni makubwa,"alisema.

Ulega alisema kwenye uvuvi yanaenda kufanywa mapinduzi makubwa kulingana na matakwa ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

"Tunafufua shirika letu la Uvuvu la TAFICO litafanya ubia na makampuni yanayoweza kufanya ubia nayo yenye mitaji mikubwa ya kibiashara kwa lengo la kukuza sekta na kuwaondoa wavuvi wetu kwenye matumizi ya vyombo duni,"alisema.

Naibu Waziri huyo alisema dhamira ya serikali ni kuhakikisha wanapata mikopo ya kuboresha ufugaji wao na vijana wengi kujiingiza kwenye shughuli hiyo.

Akitoa taarifa ya kituo atamizi,Mkurugenzi wa PASS-AIC, Tamimu Amijee, alisema kwa kipindi cha miaka miwili ya kituo hicho zaidi ya mbuzi 2500 wa kienyeji wamenunuliwa na PASS kutoka kwa wafugaji katika maeneo tofauti kwa ajili ya vijana ambao wanaendesha biashara hiyo ya unenepeshaji wa mbuzi.

# TAMISEMI yaagiza wasio na vyoo waadhibiwe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya, Dk. Grace Maghembe, amewataka maofisa afya kusimamia sheria ya usafi wa mazingira na kuwachukulia hatua kali watu wote wasio kuwa na vyoo.

Aidha, amesema kufanya hivyo kutalisaidia taifa kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza, ambayo yamekuwa mzigo kwa serikali.

Maghembe alisema hayo juzi jijini Dodoma alipokuwa akifungua mkutano mkuu wa mwaka wa afya, mazingira na usafi.

Alisema suala la mtu kuwa na choo ni jambo la lazima siyo hiyari, hivyo maofisa afya wanapaswa kusimamia sheria ya usafi wa mazingira ili kila kaya kuwa na choo bora.

Aidha, alisema hadi sasa ni asilimia 70 tu ya kaya nchini ndizo zenye huduma ya choo, hivyo jitihada za makusudi zinatakiwa kutoka kwa maofisa hao ili kufikia asilimia 100 ya kaya zenye huduma ya choo.

Alisema kama maofisa hao watazingatia usafi wa mazingira ni dhahiri magonjwa ya kuambukiza yatakwisha katika jamii kama ambavyo kipindupindu kilivyodhibitiwa mkoani Dar es Saalam.

"Asilimia 70 ya kaya zenye choo nchini bado ni kiasi kidogo sana hatupaswi kujisifu inabidi kutoka sasa kuongeza nguvu ili asilimia hii ifikie 100 hakikisheni kila kaya inakuwa na choo chake siyo kushea vyoo vya kushea ni kwenye taasisi kama vile shule, hospitali lakini siyo makazi," alisisitiza.

Alisema asilimia kubwa ya magonjwa yanasababishwa na uchafu wa mazingira kama jitihata zitawekwa kwenye sekta hiyo hali itabadilika.

"Wakati nilipokuwa mganga mkuu wa mkoa wa Dar es Saalam kipindupindu ilikuwa kila siku, lakini tulikaa na kuweka mikakati tukabaini kuwa sababu kubwa ni uchafu na kama mnavyofahamu mgonjwa wa kipindupindu ni mtu aliyekula kinyesi kwa njia yoyote ile,"alisema.

Kadhalika, alisema kutokana na jitihada hizo huu ni mwaka wa tano mkoa huo haujapata mlipuko wa ugonjwa wa kipindupindu.

Vilevile, aliwataka maofisa hao kuendelea kuwekeza katika elimu kwa jamii juu ya usafi wa mazingira na kuachana na adhabu za kuwabambikizia watu.

"Wekezeni katika elimu acheni kubambikiza faini watu wa mabucha na hoteli hiyo itakuwa biashara toeni elimu ya kutosha kwa jamii ili watu wabadilike, lakini watakaokuwa wabishi sheria itumike mara moja," alisema.

Akizungumzia kuhusu mlipuko wa virusi vya corona wimbi la nne, aliwataka maafisa hao kuendelea kuelimisha njia mbalimbali za watu kuendelea kujikinga.

Mkurugenzi msaidizi kitengo cha afya mazingira na usafi, Dk. Khalid Massa, alisema kada hiyo inakabiliwa na kero mbalimbli ikiwamo usafiri.



Baadhi ya wananchi waliojitokeza kwenye uzinduzi wa kamati ya ushauri ya kitaifa kuhusu utekelezaji wa ahadi za nchi kwenye jukwaa la kizazi chenye usawa kilichofanyika jana Jijini Dodoma ,kamati hiyo ina jumla ya watu 25 kutoka idara na sekta mbalimbali nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma yakusanya mapato kwa asilimia 35

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umekusanya mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 21.955 sawa na asilimia 35 ya makisio ya kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 64.069 zilizopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alibainisha hayo juzi alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kipindi cha kuanzia Januari hadi Novemba, mwaka huu.

Alisema Mkoa unaendelea kufanya jitihada za kuongeza makusanyo ya mapato yake ili kupanua shughuli za maendeleo.

Alisema katika ya bajeti ya mwaka 2021/22, mkoa umekisiwa kukusanya Sh. 64,069,966,000 ambapo hadi hufikia Novemba 2021 Sh. 21,954,702,178.37 zilikuwa zimekusanywa sawa asilimia 35.

Alisema kwa mwaka wa fedha 2020/21 Sh. 27,416,259,808 zilitengwa na kutolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenye halmashauri zote.

Aidha, katika bajeti ya 2021/22 makisio ya mapato ni Sh. 64,069,966,000 ambapo Sh. 42, 339, 858,025 zinatarajiwa kutengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

Aliongeza kuwa kwa pindi cha Julai hadi Novemba 2021 Sh. 9,715,664,957 zilitolewa kwa ajili ya shughuli za maendeleo.

"Hivyo kwa kipindi cha Januari hadi Novemba Sh. 37,131,924,765 zilitolewa na halmashauri zote kwa ajili ya shughuli za maendeleo"alisema

Alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22, Mkoa wa Dodoma uliidhinisha Sh. 314,667,336,350 huku kati ya hizo Sh. 128,440,880,350 ni fedha za maendeleo.

Alifafanua kuwa kati ya fedha za maendeleo Sh. 69,672,456,350 ni fedha za ndani na Sh. 58,768,424,000 fedha za nje

Vilevile, alisema hadi kufikia Novemba 2021, fedha zilizopokelewa ni Sh. 115,016,943,291.86 sawa na asilimia 33.66 ya Bajeti iliyoidhinishwa ambapo Sh. 95,589,518, 744.52 zimetumika.

Alisema Novemba Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa maendeleo ya taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19 ambapo Mkoa wa Dodoma ulipatiwa Sh. 17,667,017,106.40 hivyo kufanya Bajeti ya Mkoa kuwa Sh. 359,334,353,456.40.





# Hekta 3,000 zatengwa kwa ujenzi wa chuo kikuu

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya imetenga hekta 3,000 kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Sayansi cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Kampasi ya Mbeya.

Mbunge wa Lupa, Masache Kasaka, alisema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu hatua zilizofikiwa kutoa eneo kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho ikiwa ni ombi lililotolewa na Mkuu wa Chuo hicho, Rais Mstaafu Dk. Jakaya Kikwete wakati wa mahafali hivi karibuni jijini Mbeya.

Alisema tayari uongozi wa wilaya umeridhia ombi la kupewa eneo kwa ajili ya ujenzi wa chuo hicho na kwamba tayari wananchi wameridhia kutoa maeneo yao.

"Uwapo wa mradi wa ujenzi wa chuo hicho utawezesha kuzalisha watalaamu wengi wa afya na kuisaidia jamii kuwa na watu wenye afya njema," alisema Masache.

Alisema serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa chuo cha ufundi stadi ambao umefikia hatua za mwisho na kwamba ukikamilika utachochea vijana kupata ujuzi na kujiajiri.

Kasaka aliwahakikishia wananchi kuishawishi serikali kuleta miradi mbalimbali ya maendeleo wilayani humo ili kujikwamua kiuchumi kupitia fursa mbalimbali zitazoletwa.

Baadhi ya wadau wa maendeleo wilayani hapa walimwahidi Mbunge huyo kuendelea kutengeneza mazingira rafiki ya kuvutia wawezekaji ili kuwezesha wananchi kujiongezea kipato kupitia shughuli mbalimbali za ujasirimali.

Lawena Nsonda, mmoja wa wananchi hao, alisema katika kuunga mkono jitihada za serikali kuifanya nchi kuwa ya uchumi wa kati, ameendelea kuboresha ujenzi wa shule yake ya msingi na kuongeza wigo wa ajira ili vijana wajikwamue na umasikini na kwamba lengo ni kufungua miradi mbalimbali ya uwekezaji.



Mkuu wa wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, Dk. Vicent Anney juzi akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) juu ya mikakati ya wilaya ya kupata idadi ya walemavu kwa kila kijiji na mtaa ili Serikali iweze kuwafikia na kufahamu changamoto zao.**PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## Kanisa lasaidia wenye mahitaji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Makanisa ya Pentekoste (CPTC) wilayani Chunya, Hance Mwakibete, ameikumbusha jamii kuendelea kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu wakiwamo wagonjwa, wenye ulemavu ili kuwapa faraja na kuwasaidia kumudu gharama za maisha.

Mwakibete alitoa rai hiyo jana wakati anakabidhi mashuka 83 yenye thamani ya zaidi ya Sh. 600,000 kwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Mayeka Simon, ili kuwasaidia wagonjwa katika hospitali ya wilaya.

Alisema wameamua kuungana wachungaji wote wa makanisa ya kipentecoste wilayani hapa kufanya tendo hilo ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono serikali kuwahudumia wananchi wenye mahitaji maalumu.

"Ikiwa ni sehemu ya jamii ambayo tunaihudumia kiroho, tumejichanga kwa umoja wetu wa kanisa hili kuwaona watu wenye mahitaji mbalimbali kama vile wagonjwa na wenye ulemavu sadaka yetu haitoshi kumaliza shida zao lakini ni sehemu ya faraja kuonesha kwamba tuko nao pamoja," alisema Mwakibete.

Akizungumza mara baada ya kupokea msaada huo, Mayeka aliwashukuru wachungaji hao kuungana kwa pamoja na kuwasaidia watu wenye mahitaji maalumu.

Mayeka alisema msaada huo utasaidia kukidhi mahitaji ya wagonjwa katika hospitali ya wilaya na kwamba atahakikishia msaada huo unawafikia wagonjwa walengwa kama ilivyokusudiwa.

Pia aliwataka wauguzi kuyatumia mashuka hayo kwa malengo yaliyokusudiwa na sio vinginevyo kwa madai kuwa wachungaji wameyatoa ili kuwasaidia wagonjwa.

**"Ikiwa ni sehemu ya jamii ambayo tunaihudumia kiroho, tumejichanga kwa umoja wetu wa kanisa hili kuwaona watu wenye mahitaji mbalimbali kama vile wagonjwa na wenye ulemavu sadaka yetu haitoshi kumaliza shida zao lakini ni sehemu ya faraja kuonesha kwamba tuko nao pamoja," alisema Mwakibete.**

# CCM yataka RUWASA kutafuta suluhisho kuhusu tatizo sugu maji

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKETI wa Chama cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Mbeya, Akimu Mwalupindi, ameagiza Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani hapa, kupanua vyanzo vya maji vya Haporoto na Idimi ili kuongeza wigo wa uzalishaji maji na kuwasaidia wananchi kupata huduma hiyo kwa uhakika.

Mwalupindi alitoa agizo hilo juzi, baada ya kukagua mradi wa maji katika chanzo cha Mto Malagala - Ihango kinachohudumia vijiji vya Haporoto na Idimi.

Akiwa ameongozana na Kamati ya Siasa ya Wilaya, walianza kwa kukagua tangi lililojengwa katika kijiji cha Haporoto mwaka 2015.

Mwenyekiti huyo alisema baada ya kukagua mradi huo walibaini huduma za maji kwa watu wanaozunguka eneo hilo hazipatikani mara kwa mara hali inayosababisha wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo vijiji vya mbali. "Kamati ya Siasa ya Wilaya tunaendelea na ukaguzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Lengo ni kubaini matatizo yanayowakabili wananchi na kuangalia namna ya kutatua huku tukiambatana na wataalamu ambao hutolea ufafanuzi.

"Kiu yetu ni kuona watu wanaendelea kupata huduma safi za maji, afya, elimu na miundombinu ya barabara kwa ajili ya kurahisisha shughului zao za kujiingizia kipato," alisema Mwalupindi.

Alisema miongoni mwa miradi wanayotamani isiwe kikwazo kwa wananchi ni maji kwa sababu yameshikilia uhai wa mwanadamu hivyo upatikanaji wake utasaidia maisha kuwa rahisi kutokana na hilo aliwaomba Ruwasa kuhakikisha maji yanapatikana muda wote.

Akizungumza baada ya ukaguzi huo, Fundi Mkuu wa Maji kutoka RUWASA, Mhandisi Mwachembe Mjeni, alisema mradi huo ulikamilika tangu mwaka 2015 na kuanza kuzalisha lita 185,000 na ulitumia gharama zaidi ya Sh. milioni 700.

Naye fundi wa mradi wa maji wa Haporoto na Idimi (HAIDI), Eliud King'ala, alisema sababu kubwa ya kukwama kwa uzalishaji mkubwa wa maji kutoka kwenye chanzo cha Mto Malagala - Ihango ni shughuli za kibinadamu hasa kilimo na miti isiyo rafiki kwenye vyanzo vya maji.

Licha ya kuwapo kwa mradi huo katika vijiji vya Haporoto na Idimi , bado huduma hiyo haijafika katika Shule ya Sekondari Ihango na hatua ambayo inasababisha wanafunzi kukatisha masomo ili kufuata maji mtoni.



## SMZ yajivunia mazingira bora kwa uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imweweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wanaotaka kuwekeza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), Sharif Ali Shari, aliyasema hayo jana ofisini kwake, Maruhubi, wakati akizungumza na ujumbe wa kampuni ya Hoteli za Triumph kutoka Misri.

Alisema serikali imejenga misingi imara kwa wawakezaji wenye nia ya kuwekeza Zanzibar na imejipanga katika kuhakikisha wawakezaji wanaoingia nchini wanakuwa salama na mali zao pamoja na wanachokiwekeza.

Sharif alisema uamuzi wa ujumbe huo kutoka Misri kuwekeza Zanzibar katika mambo ya kilimo , uvuvi na hoteli ni mzuri na akapongeza kwa hatua hiyo.

Mkurugenzi huyo alisema ujumbe huo umeonyesha nia ya kujenga hoteli ya nyota tano katika maeneo ya Maisara mjini Unguja na Kibwengo mkoa wa Kaskazini Unguja ambayo ni moja ya sehemu nzuri za kuwekeza katika utalii.

Naye mwenyeji wa ujumbe huo ambaye ni Mkuu wa Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) Komodore Azani Hassan Msingiri, alisema wawekezaji hao wamekuja kutokana na mazungumzo aliyoyafanya na balozi wa Misri kipindi kilichopita .

Alisema ameamua kufanya hivyo kutokana na kauli ya Rais wa Zanzibar kuwapa nafasi ya kuwatafuta wawekezaji katika taasisi zao na kwamba ujumbe huo umevutiwa sana kuona hali halisi ya usalama ilivyo katika visiwa vya Zanzibar .

Ujumbe huo umeongozwa na Meja Jenerali Ehab Shoman kutoka Misri na kusema kuwa amevutiwa zaidi na hali ya mazingira ya Zanzibar .

"Hali halisi ya kisiwa cha Zanzibar kinaonekana kuwa ardhi nzuri ya kuwekeza na katika, utalii, kilimo na uvuvi wa bahari," alisema Jenerali Shomon.

# Wizara yaweka mikakati matumizi mabwawa kujitosheleza kwa chakula

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imesema imeweka mikakati kuliimarisha bonde la mpunga la Bumbwisudi wilaya ya Magharibi, Unguja ili kujitosheleza kwa chakula.

Hayo yaliyasemwa jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi na Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Soud Nahoda, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said.

Machano katika swali hilo, alitaka kujua Wizara imejipanga vipi katika kuhakikisha kuona Zanzibar inajitosheleza kwa chakula kwa kuyatumia mabonde ya mpunga yaliyopo likiwamo la Bumbwisudi.

Akijibu swali hilo, Waziri Nahoda alisema wizara imejipanga kuendeleza bonde hilo katika kilimo cha umwagiliaji na kwa sasa ekari 210 zinalimwa na wakulima wa aina mbalimbali.

Waziri alisema katika mpango mkuu wa kilimo cha umwagiliaji, wizara inaendelea na mikakati yake ya kutafuta wawekezaji wa aina mbalimbali kuwekeza maeneo ya mabonde mengine.

Alisema kwa sasa bonde la Bumbwisudi liko chini ya wizara huku likiwa na zaidi ya maeneo 15 pamoja na wataalamu saba wa kilimo ambao wamekuwa wakifanya kazi karibu na wakulima katika kuwapatia mbinu za kisasa za kilimo chenye tija.

Nahoda aliyataja maeneo hayo kuwa ni Kitundu, Langoni, Mkanyageni na Popo na kwamba kwa sasa kazi za uchimbaji wa visima na ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji inaendelea.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya ,Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia, na Watoto Fatma Mrisho akizungumza kuhusu hospitali 10 za wilaya ambazo zitajengwa maeneo mbalimbali Unguja na Pemba ,mara baada ya kusaini mikataba ya makubaliano ya ujenzi wa hospitali hizo na wakandarasi wa kampuni mbalimbali za ujenzi , ofisini kwake Mnazi mmoja mjini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Viongozi wa dini watakiwa kufuata sheria usimamizi majukumu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amewashauri viongozi wa dini kufuata sheria na kanuni katika kusimamia majukumu yao.

Hemed aliyasema hayo jana ofisini kwake, Vuga Mjini Zanzibar alipokutana na kufanya mazungumzo na Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini iliyo chini ya Mwenyekiti wake Mufti wa Zanzibar.

Alisema kuna haja kwa viongozi wa kamati hiyo kusimamia sheria hasa kwa kuzingatia imani za dini ili kuwa karibu na Mungu jambo ambalo litasababisha kuwa na jamii yenye imani.

Hemed alisema si jambo la kuridhisha kwa baadhi ya watu wenye nia mbaya kwa kujivika vazi la viongozi wa dini hali ya kuwa kamati inayotambulika kisheria iko chini ya usimamizi wa ya Ofisi ya Mufti wa Zanzibar.

Alisema serikali inathamini mchango unaotolewa na kamati hiyo na itaendelea kutoa kila aina ya ushirikiano ili kuhakikisha inaendelea kufanya kazi vyema.

Sambamba na hilo, aliwakumbusha viongozi hao kutumia nafasi waliyo nayo katika jamii kwa kuendelea kuhubiri amani hasa katika maeneo yao ya ibada na kwamba jamii inawaamini na kuwasikiliza.

Hemed pia alisema maendeleo katika nchi yoyote ili yapatikane ni lazima pawe na amani na kubainisha kwamba serikali imekuwa ikihamasisha amani na utulivu. Alisema hadi sasa wananchi wamekuwa waelewa katika kulinda tunu hiyo na kwa sasa serikali inaendeleza kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mjumbe wa Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini, Mchungaji Shukuru Maloda, alisema kamati hiyo inaunga mkono serikali katika kupiga vita udhalilishaji na mwaka 2022 imeandaa mkakati madhubuti itakaoouanza kwa wilaya za Kati Unguja na Micheweni, Pemba kuhakikisha vitendo hivyo vinapungua.

Naye Mjumbe wa Kamati hiyo, Sheikh Thabit Nouman Jongo, alisema miongoni mwa kazi za kamati hiyo ni kutatua migogoro katika jamii na kuhamasisha amani. Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini Zanzibar ilianzishwa mwaka 2005 chini ya aliyekuwa Mufti wa Zanzibar, Marehemu Sheikh Harith bin Khelef.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA** Nyumba inauzwa Morogoro Mjini Masika Mil. 100. Ni nzuri kwa biashara, ina vyumba kumi na nne. Kwa mawasiliano piga simu namba: 0745 222 312 / 0715 768 811.

OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI, INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0782253676

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya MASWA.**

**Kituo cha NYALIKUNGU mkoa wa SIMIYU**
**Usimamizi wa Mirathi Na.34/2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU GERVAS KADALA WA MALAMPAKA-MASWA.**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA DENNIS JULIUS KADALA**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 22 Mwezi Desemba Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia:**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuleta mahakamani kukaguliwa.

Imetolewa leo tarehe 15 Mwezi 12 Mwaka 2021.

116620302

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**

**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo ………..PONGWE WILAYA TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi…………….53…………2021**

**Ombi la…………REHEMA D/o SHABANI ……..Kuteuliwa**

**Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu …….SHABANI D/o WAMBUA…….**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/12/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 7/12/2021

116620402

---

**FOMU MADAI -3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**

**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**

**Shauri la Madai / Ndoa Na 60, 2021**

**Jina la Mdai Abeid Jalala Sudi**

**Jina la Mdaiwa Binuti Zuberi Suleiman**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: Binuti Zuberi Suleiman**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai )**

Mdai anadai talaka dhidi yako hivyo fika mahakamani kujibu madai hayo Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 21 mwezi 12 mwaka 2021 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 13 mwezi 12 Mwaka 2021

HAKIMU

116620502

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VALENTINE LEOPOLD NDANU**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T125BEL**

Chassis namba **01250318**

Engine namba **5759970**

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu

Taarifa ya Polisi –

**ARU/ARU/RB/588886/2021**

116620702

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Morogoro**

**Kituo cha KINGOLWIRA Mkoa Wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi Na……26..2021**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU SHABAN NASSORO KIPANDE WA KINGOLWIRA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA KIPANDE SHABANI NASSORO**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 11 Mwezi 12 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

**Imetolewa Tarehe 15 Mwezi 12Mwaka 2021**

116620802

---

**PAMOJA DISPENSARY LTD**

**Affiliated to Now for Compassion (NFC) Tanzania**

**PAMOJA DISPENSARY LIMITED**

**NOTICE OF FINAL GENERAL MEETING**

**(Section 345 of the companies Act, 2002)**

Notice is hereby given in accordance with section 345 (2) of the companies Act, 2002 that the final General meeting of the company will be held on the 10th day of December, 2021 from 11:00am at the company's registered office at Ngaramtoni-Oloirien village, Arusha. The purpose of the meeting will be:

1. Receiving an account laid before them showing the manner in which the winding up of the company has been conducted and its property disposed of arid that the same was done accordingly and hearing any explanation that may be given by the liquidator.
2. By resolution determining the manner in which the books, accounts and documents of the company and the liquidator shall be disposed of and:
3. By resolution dissolving the company.

Dated on this 02th day of December, 2021

JACQUELINE MWENZEGULE
LIQUIDATOR

116621302

---

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa**

**Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Faru 24 wauawa Afrika Kusini kwa siku 14

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

VIFARU 24 wameuawa Afrika Kusini kwa takriban wiki mbili, wizara ya mazingira imethibitisha.

Inasema mizoga saba, ilipatikana katika Hifadhi ya Kitaifa ya Kruger, mingine saba katika jimbo la Mpumalanga, sita KwaZulu-Natal na minne Cape Magharibi.

Wizara hiyo imelaani kuendelea kwa ujangili na mauaji ya vifaru kwa ajili ya pembe zao, ikisema washukiwa tisa wa uhalifu huo, wamekamatwa katika siku 14 za kwanza za mwezi wa Desemba.

Imewahimiza wananchi kusaidia kwa taarifa zozote zinazoweza kusababisha kukamatwa na kufunguliwa mashtaka kwa majangili.

Afrika Kusini ni makao ya karibu asilimia 80 ya idadi ya vifaru barani Afrika, ambayo iko chini ya 30,000.

Mamia huuawa kila mwaka kwa ajili ya pembe zao, nyingi kati yake zikielekea Asia ambako pembe za faru ni kiungo katika dawa na tiba asilia.

Idara ya mazingira ilisema itatoa taarifa kuhusu jumla ya idadi ya vifaru waliouawa kwa ajili ya pembe zao mwaka wa 2021 mapema mwaka wa 2022.

**BBC**

# Waandishi 488 wafungwa jela, 46 wauawa 2021

**Paris,** UFARANSA

SHIRIKA la Waandishi Habari Wasiokuwa na Mipaka (RSF), limesema hadi sasa kuna waandishi wa habari 488, waliofungwa jela kote duniani.

China inaongoza katika nchi zilizowafunga waandishi habari ikiwa na 127.

Linasema hiyo ni idadi kubwa zaidi, tangu shirika hilo lilipoanza kuorodhesha matukio hayo miaka 25 iliyopita.

RSF linasema idadi ya waandishi waliouawa mwaka huu ni 46, ikiwa ni ya chini tangu lilipoanza kutoa takwimu za kila mwaka, kutokana na kutulia kwa kiasi fulani kwa mizozo katika eneo la Mashariki ya Kati.

Taarifa ya shirika hilo linalopigania uhuru wa waandishi wa habari, ilisema idadi ya waliokamatwa imeongezeka kwa asilimia 20 ya mwaka uliopita, kwa kiasi kikubwa kutokana na ukandamizaji dhidi ya vyombo vya habari nchini Myanmar, Belarus na Hong Kong.

Pia, shirika hilo lilisema kuwa halijawahi kuona waandishi habari wa kike wakikamatwa kama ilivyo sasa, idadi yao waliokamatwa ni 60 kwa sasa, likitaja ni ongezeko la zaidi ya asilimia 30 ikilinganishwa na mwaka 2020.

**DW**

# Mchungaji adai upendo sababu kushiriki ngono na mwanakwaya

**Lagos,** NIGERIA

MCHUNGAJI wa kanisa la Christ Apostolic Bible katika jimbo la Ogun lililopo Kusini Magharibi mwa Nigeria, anaendelea kushikiliwa mahabusu tangu Ijumaa, baada ya kudaiwa kumbaka msichana wa miaka 16.

Polisi katika jimbo la Ogun, wanaochunguza tukio hilo wanasema mchungaji huyo alipanga na mke wake kumbaka msichana huyo ambaye ni mwanakwaya katika kanisa lao.

Mchungaji Peter Taiwo na mke wake, wanakwepa kueleza ukweli halisi wa kilichotokea.

Mchungaji huyo anasema yeye na msichana huyo wamekuwa katika mapenzi na wote walipendana kimapenzi.

"Nilimwambia aachane na mpenzi wake wa kiume na aniombe chochote anachohitaji."

Mchungaji huyo alisema wakati msichana alipoumia mguu, aliwasaidia wazazi wake kupata usaidizi wa matibabu yake.

"Kuanzia siku nilipouangalia mguu wake, msichana alianza kunitumia jumbe za mapenzi na nilikuwa nazijibu. Bado nina jumbe katika simu yangu ," alisema Mchungaji.

"Tuliongea nikamwambia hakuna kushiriki ngono pamoja, lakini tumekuwa tukipendana", alisema Mchungaji na kuongeza: Wakati ule tulipoanza hatukuwa na mahusiano ya kingono, lakini tulionyeshana mapenzi," Pasta Taiwo alisema.

Hata hivyo mchungaji anakiri kuwa waliingia katika mahusiano ya ngono na msichana na kumfahamisha mke wake, ambaye hakuwa na la kusema.

Akizungumza na BBC mke wa Mchungaji alisema hakuwa anafahamu kuwa mume wake alikuwa anamtumia vibaya msichana.

**BBC**



Profesa Patricia Kingori wa Chuo Kikuu Oxford nchini Uingereza. Mmoja wa wanawake wachache, wenye umri mdogo zaidi kuwahi kutunukiwa Uprofesa kamili katika historia ya miaka 925. **PICHA: MAKTABA**

# Mwafrika aweka rekodi ya karne 9 kutunukiwa 'uprofesa' Oxford

**Londo,** UINGEREZA

MWAFRIKA mwenye asili ya Kenya, amekuwa profesa wa kwanza mweusi na umri mdogo katika chuo kikuu cha kifahari Uingereza, Oxford University, imesema taasisi hiyo ya elimu.

Takwimu zinaonyesha kuwa ni asilimia moja ya maprofesa wa vyuo vikuu vya Uingereza ni weusi.

Patricia Kingori, pia ni mmoja wa wanawake wachache, wenye umri mdogo zaidi kuwahi kutunukiwa Uprofesa kamili katika historia ya miaka 925 ya chuo kikuu cha Oxford.

Profesa Kingori, ambaye ni mwanasosholojia aliyebobea katika masuala ya wahudumu wa afya, alieleza kufurahishwa kwake na uteuzi huo

"Kutambuliwa kwa kazi yangu kwa njia hii ni heshima kubwa na ninawashukuru sana watu niliojifunza kutoka kwao na walionisaidia hadi sasa," alisema.

Pia aliwahi kuwa mshauri wa mashirika kadhaa ya kidunia, ikiwa ni pamoja na Shirika la Afya Duniani (WHO), Save the Children na Médecins Sans Frontières (MSF).

Kingori, ambaye alikulia katika kisiwa cha Caribbean cha St Kitts kulingana na chanzo cha habari cha eneo hilo, amekuwa akielezewa kama mbunifu na mwanamke jasiri kutoka Chuo kikuu cha Somerville.

Kufikia mwezi Januari mwakani, ni maprofesa 155 pekee kati ya zaidi ya 23,000 wa chuo kikuu Oxford, waliokuwa ni weusi, kwa mujibu wa takwimu rasmi.

**BBC**

# BADRU AFUNGUKA SIRI YA USHINDI AZAM FC

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Green Warriors na kusonga mbele katika mashindano ya Kombe la FA, Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Mohammed Badru, amesema kazi kubwa aliyoifanya katika kikosi chake ni kuwaweka vyema kisaikolojia wachezaji wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, Badru alisema morali ya wachezaji wa Azam FC ilikuwa chini kutokana na matokeo mabaya waliyopata katika mechi zilizopita na si kwamba kikosi hicho kina uwezo mdogo.

Badru alisema Azam ina wachezaji wazuri na wenye uwezo mkubwa, lakini matokeo waliyokuwa wanapata yalitokana na akili yao haikuwa imetulia.

"Naamini kisaikolojia wachezaji hawakuwa vizuri, akili ikipanguka wachezaji hawawezi kucheza vizuri, tulichofanya kwa siku hizi mbili ni kuwaweka vizuri kisaikolojia, ndio maana unaona matokeo yamekuwa mazuri," alisema Badru.

Kocha huyo alikiri hawezi kujisifia kutokana na ushindi wa juzi kwa sababu timu yake ilikutana na wapinzani dhaifu 'kidogo' na sasa ameanza kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya mechi za Ligi Kuu ambapo Jumamosi watawakaribisha Mbeya City kwenye Uwanja wa Azam Complex.

"Tuna mechi tatu mfululizo, hivyo katika mechi hizo ndiyo tutaangalia timu inabadilika vipi, tunataka tukusanye pointi tisa kwenye michezo hiyo ili kujiweka vizuri katika msimamo wa ligi," Badru alisema.

Aliongeza anaamini timu yao itaanza kucheza soka la ushindani na kurejea kwenye mbio za kuwania taji la ligi ambalo kwa sasa linashikiliwa na Wekundu wa Msimbazi.

"Bado hatujafanya vibaya sana, wachezaji wanahitaji utulivu, hili likirejea, moto wetu utaonekana," aliongeza kocha huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar na Gwambina FC.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania inayofuata ya Azam itakuwa ni dhidi ya Ruvu Shooting itakayochezwa Desemba 23, mwaka huu huku ikimfuata Simba Januari Mosi mwakani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Badru amepewa mikoba ya kuiongoza Azam FC baada ya mabosi wa timu hiyo kuachana na Mzambia George Lwandamina kutokana na kutopata matokeo chanya.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hassan Abbas (kushoto), akimkabidhi zawadi mshindi wa muziki wa kizazi kipya, Abisai Kassanga kutoka Pwani katika shindano la Taifa Cup Music Challenge lililofanyika jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MTANDAO**

# Wauzaji jezi feki 11 wakamatwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JESHI la Polisi limewakamata wafanyabiashara 11 na kuwafungulia mashtaka kuhusiana na tuhuma za utengenezaji wa jezi feki kwa msaada kutoka kwa viwanda vinavyotengeneza jezi hizo halisi.

Mbali na hilo, jeshi hilo limekamata jezi feki za Simba 279 pamoja na watuhumiwa 15 kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Mwanza, Tabora na Tunduma ambao walikutwa na jezi hizo wakiziuza.

Akizungumza jijini hapa jana, Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alisema watu hao pia wamekamatwa na urembo wa shingo za jezi 300.

Misime alisema ufanyaji wa kosa hilo ni kuidhulumu serikali mapato kutokana na ukwepaji wa kulipa kodi wanaofanya.

"Kama inavyofahamika baadhi ya timu huingia mikataba na kampuni kwa ajili ya utengenezaji wa jezi kwa makubaliano rasmi na jezi zinapouzwa kiasi fulani cha fedha hupatiwa kwa ajili ya kulipa mishahara ya wachezaji na huduma nyingine," Misime alisema.

Amewataka wananchi kuendelea kutoa taarifa pale wanapoona jezi feki zinauzwa ili kukomesha tabia hiyo mara moja.

## Mjini Magharibi mabingwa netiboli

**Na Saada Akida**

TIMU ya netiboli ya Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja Visiwani Zanzibar wameibuka mabingwa wa Samia Taifa Cup katika mchezo huo baada ya kuifunga Dar es Salaam magoli 41-32 kwenye fainali iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ndani wa Benjamini Mkapa jijini jana.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Yusuph Singo, alisema kupitia mashindano hayo wameona vipaji vingi.

Singo aliwapongeza Mjini Magharibi kwa kutwaa ubingwa huo na kuongeza walionyesha ushindani na kiwango kizuri dhidi ya wapinzani wao.

"Kwa jinsi nilivyoona timu ya Mjini Magharibi ilivyoleta ushindani, imedhihirisha jinsi gani nchi hii ina vipaji vingi, kupitia Samia Taifa Cup,... baada ya mashindano haya serikali ina mpango wa kuendeleza mchezo huu ili kuhakikisha unafanya vizuri katika michuano ya kimataifa," alisema Singo.

Kocha wa Mjini Magharibi, Ramadhani Zimbwe, alisema siri kubwa ya kutwaa ubingwa huo ni wachezaji wake kujituma na kucheza kitimu iliwasaidia kufikia malengo hayo.

Zimbwe alisema wanashukuru kuona malengo yao ya kucheza fainali na kutwaa ubingwa kwa mwaka huu yametimia lakini hakuacha kuwapongeza Dar es Salaam kwa kueleza walikuwa na kikosi 'kigumu'.

## Nyota wa zamani Olimpiki waitwa

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

WANAMICHEZO wastaafu waliowahi kushiriki Michezo ya Olimpiki wametakiwa kuisaidia Tanzania ili ifanye vizuri katika michezo mbalimbali ya kimataifa, imeelezwa.

Rais wa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC), Gulam Rashid, amesema hayo jana wakati akifungua Mkutano Mkuu wa kwanza wa Kamati ya Wachezaji (Kawata).

Gulam alisema endapo wanamichezo hao watashirikiana kikamilifu katika kuendeleza michezo katika vyama na mashirikisho ya michezo waliyoshiriki Olimpiki, basi watasaidia kuondoa changamoto zinazowakabili wanamichezo waliofuzu.

Kiongozi huyo alisema wanamichezo wastaafu wanatakiwa kutoa ushauri wa namna bora ya kuendesha shughuli za michezo ili kufikia malengo ya ushindi kama wanavyofanya wenzao katika mataifa mengine.

Katibu Mkuu wa TOC, Filbert Bayi alisema ni muhimu kuona vyama vya michezo vinakuwa na kamisheni zake za wachezaji ili kusaidia kuondoa changamoto katika mchezo wao.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TRIPPIER KITAELEWEKA
NEWCASTLE United wanazidi kuwa na uhakika wa kumsajili beki wa Timu ya Taifa ya England, Kieran Trippier, mwenye umri wa miaka 31, kutoka Atletico Madrid ifikapo Januari. ***(Football Insider)***

### TUCHEL AMKATAA AUBAMEYANG
KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amesema atawasiliana na Pierre-Emerick Aubameyang baada ya mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Gabon mwenye umri wa miaka 32, kuvuliwa unahodha wa Arsenal. ***(Mirror)***

### HAALAND AELEKEA BARCA
BARCELONA wanajiandaa kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21.***(Sport)***

### CITY YAMFUATA HAALAND
KLABU ya Manchester City nayo imeonyesha kuvutiwa na Erling Haaland, lakini wanaweza kutokuwa tayari kutumia fedha za kutosha kumpata mshambuliaji huyo. ***(Manchester Evening News)***

### VLAHOVIC AGOMBEWA EPL
KLABU za Arsenal, Tottenham na Manchester United zipo tayari kumtaka Dusan Vlahovic baada ya kupata habari za mshambuliaji huyo wa Serbia mwenye umri wa miaka 21 amekataa "mkataba wa juu zaidi katika historia ya Fiorentina".***(Talksport)***

### RUDIGER: NAONDOKA CHELSEA
MLINZI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, ambaye amebakiza miezi sita katika mkataba wake, amethibitisha anafikiria kuondoka katika klabu hiyo Januari.***(Sky Sports via Mirror)***

### KLOPP AMZUIA GOMEZ
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema mlinzi wa England, Joe Gomez mwenye umri wa miaka 24, hataondoka na kujiunga na Steven Gerrard kule Aston Villa katika dirisha la uhamisho la Januari.***(Express)***

### HAIDARA ANUKIA UNITED
KIUNGO wa kati wa RB Leipzig, Amadou Haidara mwenye umri wa miaka 23, amechochea uvumi unaomhusisha na Manchester United baada ya kumsifu kocha wa muda wa klabu hiyo, Ralf Rangnick. ***(Bild,via Express)***

### SANCHEZ MAMBO MAGUMU
MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Alexis Sanchez mwenye umri wa miaka 32, anaweza kurejea Barcelona kwa mkopo, huku mshambuliaji, Luuk de Jong mwenye umri wa miaka 31, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Barca kutoka Sevilla, akihamia Inter.***(Sport)***

### PHILLIPS ATOA MSIMAMO
MLINZI Nat Phillips mwenye umri wa miaka 24 amekiri yuko tayari kuondoka Liverpool Januari.***(Sky Sports,via Liverpool Echo)***

### MIDDLESBROUGH YAJIPANGA
KLABU ya Middlesbrough ipo kwenye mazungumzo ya kusajili washambuliaji wawili kwa mkopo mwezi ujao. ***(Football Insider)***

### SENESI ANUKIA ENGLAND
WEST Ham ni miongoni mwa klabu za Ulaya zinazotaka kumsajili mlinzi wa Timu ya Taifa ya Argentina anayechezea Feyenoord, Marcos Senesi mwenye umri wa miaka 24. ***(90min)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: LACAZETTE AMEONYESHA UKOMAVU

Ni katika nafasi yake mpya aliyoshika kwenye kikosi cha Arsenal ambacho…

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesifia nguvu ya nahodha, Alexandre Lacazette wakati akielezea namna wachezaji wake walivyoonyesha kiwango cha kuvutia wakati Arsenal ikishinda mabao 2-0 dhidi ya West Ham katika mchezo wa Ligi Kuu England uliochezwa juzi.

Lacazette, ambaye penalti yake ya kipindi cha pili iliokolewa na Lukasz Fabianski, alivaa kitambaa cha unahodha katika mchezo huo baada ya Pierre-Emerick Aubameyang kuvuliwa wadhifa huo kutokana na kuvunja "sheria za kinidhamu."

Kikosi hicho cha Arteta kilitawala mchezo wote na Gabriel Martinelli alikiweka mbele kwa kufunga bao lake la saba msimu huu.

Emile Smith Rowe aliyetokea benchi alifunga bao la ushindi na kuwawezesha washikabunduki hao kuondoka na pointi zote tatu.

Arsenal sasa imejiweka kwenye nafasi ya kuwania kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa ushindi huo na Arteta alisifia uongozi wa wachezaji wakubwa baada ya timu hiyo kupata ushindi wake wa 11 kati ya mechi 12 dhidi ya wagonga nyundo hao wa London.

"Nafikiri walikuwa vizuri sana na wachezaji wakubwa walionyesha mfano," alisema Arteta akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulipata mabao. Ni muhimu kwa Gabi (Martinelli) kufunga bao kama lile. Nimeridhishwa na kila mmoja.


"Wachezaji wanacheza kwa ajili ya klabu na wanajisikia fahari kwa kile tulichotarajia kutoka kwao.

"Nilikuwa na furaha sana tangu kipindi cha kwanza, kwa sababu tulijua tunatakiwa kucheza vizuri ili kuifunga West Ham."

Akizungumzia kiwango cha Lacazette, Arteta aliongeza: "Alikuwa kwenye nafasi nzuri na alionyesha nguvu yake ya unahodha, kwa namna kila mmoja alivyocheza leo (juzi) tulikuwa na furaha kubwa na alionyesha kuhimili majukumu yake. Kwa uhakika najisikia fahari kwa majukumu yake."

MECHI KALI
HOME AWAY
BAYERN MUNCHEN
1.17 | 7.59 | 12.98
VFL WOLFSBURG
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 783
KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# POGBA AKATALIWA BARCELONA



**LONDON, England**

TAARIFA zinasema, Rais wa Barcelona, Joan Laporta, amekataa kumsajili nyota wa Manchester United, Paul Pogba, katika mazungumzo yake na wakala wa nyota huyo, kwa mujibu wa ESPN.

Wakala, Mino Raniola na Laporta walipata fursa ya kuonana Jumanne, na wakafanya mazungumzo juu ya biashara za majina kadhaa ya wachezaji, huku jina la Pogba pia likiibuka kwenye mazungumzo yao.

Nyota huyo wa Ufaransa anatazamia kuwa mchezaji huru msimu ujao wa joto, wakati mkataba wake wa sasa ukiwa ukingoni.

Licha ya ugumu wa swali la uwezo wa Barcelona kufikia gharama ya mshahara wa Pogba, Barca wanaonekana hawana kabisa mpango naye.

Kwa mujibu wa Sport, Laporta ametajwa amemwambia Raniola kuwa Pogba hatakiwi pale Camp Nou.

Sababu kubwa inayotajwa ni kuwa Barca hawaoni kama anafaa kwenye aina ya kiungo ambaye kocha mkuu, Xavi Hernandez anayemhitaji.

Kwa mujibu wa bosi huyo, Xavi anahitaji kiungo mwenye umbo la kawaida na mwenye ufundi zaidi kuliko matumizi ya mwili.

Pogba licha ya ufundi aliojaliwa, pia hutumia nguvu zaidi mchezoni na Xavi anahitaji kitu tofauti hivyo nyota huyo hakidhi vigezo.

# Dortmund, Chelsea zapambana kwa Ziyech



**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU ya Borussia Dortmund imeripotiwa inataka kujaribu kufukuzia saini ya nyota wa Chelsea, Hakim Ziyech.

Katika msimu ambao amekuwa akipambana na majeraha, Ziyech amecheza mechi 11 huku michezo mitano akitokea benchi katika mashindano yote.

Hata hivyo, taarifa zaidi zinasema raia huyo wa Morocco anatatizwa na kukosa muda wa kutosha wa kucheza katika kipindi cha kwanza cha msimu.

Kwa mujibu wa Bild, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 "hajaridhishwa" na hali yake pale, Stamford Bridge na yuko tayari kuondoka the Blues hapo.

Dortmund inadaiwa kumtambua Ziyech kama kipaumbele chao wakati wa dirisha dogo la Januari huku wakitaka kupambana na vinara wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich.

Hata hivyo. bila kujali kama ni dili la kudumu au la mkopo kwa Ziyech, kocha mkuu wa Chelsea, Thomas Tuchel anatarajiwa kukataa kutengana na mchezaji huyo ambaye amemsifu sana katika wiki za hivi karibuni.

**HABARI MICHEZO**

# 3,781,040

# JACKPOT MECHI WIKI HII

**BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13**

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/12/2021 | 18:00 | Bristol City vs Huddersfield | 2.69 | 3.18 | 2.54 |
| 02. 18/12/2021 | 18:00 | Watford vs Crystal Palace | 2.89 | 3.34 | 2.41 |
| 03. 18/12/2021 | 20:30 | Leeds vs Arsenal | 2.97 | 3.41 | 2.32 |
| 04. 18/12/2021 | 22:45 | Cagliari vs Udinese | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 05. 18/12/2021 | 23:00 | Sevilla FC vs Atletico Madrid | 2.65 | 3.00 | 2.85 |
| 06. 19/12/2021 | 15:00 | Everton vs Leicester | 2.75 | 3.30 | 2.55 |
| 07. 19/12/2021 | 16:00 | Granada vs Mallorca | 2.49 | 3.14 | 2.94 |
| 08. 19/12/2021 | 16:00 | Fuenlabrada vs Real Oviedo | 2.90 | 3.05 | 2.45 |
| 09. 19/12/2021 | 17:00 | Spezia vs Empoli | 2.40 | 3.49 | 2.79 |
| 10. 19/12/2021 | 17:30 | SC Freiburg vs Bayer Leverkusen | 2.79 | 3.44 | 2.40 |
| 11. 19/12/2021 | 18:00 | Zaragoza vs Tenerife | 2.38 | 3.08 | 2.98 |
| 12. 19/12/2021 | 20:30 | Getafe vs Osasuna | 2.49 | 2.90 | 3.20 |
| 13. 19/12/2021 | 22:45 | AC Milan vs Napoli | 2.37 | 3.41 | 2.91 |

# MAKAMBO AANZA TAMBO YANGA

**Na Dennis Fussi**

MSHAMBULIAJI Yanga, Heritier Makambo, ametimiza ahadi ya kuonyesha makali katika mchezo wa Kombe la FA dhidi ya Ihefu baada ya kufunga mabao matatu peke yake.

Yanga iliibuka na ushindi kwa mabao 4-0 na kusonga mbele katika mchezo huo huku goli lingine likifungwa na Khalid Aucho, juzi Jumatano.

Akizungumza na gazeti hili kabla ya mchezo huo, Makambo alisema endapo kocha Nasriddine Nabi angempa nafasi ya kuanza kwenye mchezo huo wa raundi ya tatu angeonyesha uwezo wake.

Makambo alisema alijiandaa vyema kuhakikisha anaibeba timu yake kwa kufungua akaunti yake ya mabao msimu huu.

"Sijafunga bao tangu nirudi tena Yanga, na kwenye mechi za ligi sipati muda wa kutosha wa kucheza naamini hii ndio mechi yangu ya kuanza na kumuonyesha kocha nilichokuwa nacho," alisema Makambo kabla ya mchezo huo.

Bingwa mtetezi wa mashindano hayo ambayo hutoa tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ni Simba.




Mshindi wa SportPesa Jackpot bonus, Kassim Liuzilo (52), kutoka Kilombero, Morogoro akishikilia mfano wa hundi ya Sh. milioni 10.3 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya wiki iliyopita. Jackpot inayoshindaniwa wiki hii ni 783,781,040/-. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kifaru: Moto wetu hautapoa

**Na Dennis Fussi**

BAADA ya kupata ushindi wake wa kwanza kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United na juzi kuifumua Tunduma United mabao 7-1 katika Kombe la Shirikisho, Mtibwa Sugar sasa 'haipoi na gari imeshawaka'.

Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru, aliliambia gazeti hili 'moto'ilioanza nao timu hiyo kwa sasa, hautapoa na wataendelea kuwa kwenye kiwango hicho katika mechi zote zinazofuata.

Akizungumza kuelezea mchezo huo dhidi ya Tunduma uliopigwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex ulioko Turiani mkoani Morogoro, Kifaru amesema kurudi kwao kwenye dimba la nyumbani kumewafanya kuwa na ari kubwa mno.

"Unajua huu ni mchezo wetu wa pili tunacheza kwenye uwanja wetu wa nyumbani baada ya kufunguliwa na pia ni ushindi wetu wa pili msimu huu, ninachoweza kusema ni moto huu hautazima, tutaendelea kwa mechi zote zinazofuata," alisema Kifaru.

Aliongeza; "Tulianza msimu vibaya kwa kupoteza mechi tano na sare mbili, lakini sasa tumerudi kwenye kiwango chetu na kikubwa zaidi tunacheza mbele ya mashabiki wetu ambao watupa ari kubwa sana na ndio maana tunashinda kwa urahisi."

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

**IJUMAA - 17 - DESEMBA 2021**


| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2528 | Maccabi Jaffa vs SC Kfar Qasem | 4.63 | 3.47 | 1.68 |
| 14:00 | 2817 | Geita Gold FC vs Ruvu Shooting | 2.09 | 2.81 | 3.77 |
| 14:00 | 5427 | Ironi Tiberias vs Bnei Sakhnin | 5.97 | 4.24 | 1.44 |
| 15:00 | 1253 | Ahi Nazareth vs Hapoel Acre | 2.51 | 3.09 | 2.65 |
| 15:00 | 3878 | Welayta Dicha FC vs Saint George FC | 2.70 | 2.89 | 2.60 |
| 15:00 | 4226 | FC Ashdod vs El Fahem | 1.50 | 4.04 | 5.38 |
| 15:00 | 5540 | Bul FC vs Bright Stars | 1.51 | 3.76 | 5.78 |
| 15:00 | 5734 | Mbarara FC vs Wakiso Giants FC | 2.70 | 3.25 | 2.60 |
| 15:40 | 4501 | Al-Thaid vs Masafi | 2.15 | 3.71 | 2.74 |
| 15:40 | 5639 | AL-Rams vs AL Arabi | 7.15 | 5.02 | 1.31 |
| 15:45 | 1850 | Al-Hamriyah vs City Football Club | 1.24 | 5.58 | 8.66 |
| 15:45 | 5028 | AL Bataeh (UAE) vs Hatta Club | 2.22 | 3.70 | 2.64 |
| 16:00 | 5783 | Mbeya Kwanza FC vs Namungo | 2.40 | 2.75 | 3.13 |
| 17:00 | 1788 | ASO Chlef vs USM Alger | 3.23 | 2.84 | 2.28 |
| 17:00 | 1807 | MC Magra vs RC Arbaa | 1.49 | 3.66 | 6.36 |
| 17:25 | 4743 | Al Shabab Kuwait vs AL Nasr | 4.43 | 3.56 | 1.68 |
| 18:00 | 2040 | MC Oran vs US Biskra | 1.81 | 3.32 | 4.05 |
| 18:00 | 2426 | Nea Salamis vs Alki Oroklini | 2.51 | 2.95 | 2.76 |
| 18:00 | 3477 | Enyimba vs Abia Warriors FC | 1.27 | 4.73 | 9.65 |
| 18:00 | 3492 | RS Berkane vs Rapide Oued Zem | 1.42 | 4.14 | 6.55 |
| 18:00 | 3699 | Wolkite City FC vs Ethiopia Bunna SC | 2.79 | 2.93 | 2.50 |
| 18:15 | 5829 | Tshakhuma vs Amazulu | 2.99 | 2.84 | 2.55 |
| 19:00 | 4836 | Dunajska Streda vs Ruzomberok | 1.45 | 4.15 | 5.98 |
| 19:00 | 5978 | Dodoma FC vs Polisi Tanzania | 2.31 | 2.70 | 3.37 |
| 20:00 | 3850 | Wisla Krakow vs Nieciecza KS | 1.89 | 3.38 | 3.62 |
| 20:00 | 5062 | Slaven Belupo vs Lokomotiva Zagreb | 2.84 | 3.28 | 2.26 |
| 20:00 | 5175 | Giresunspor vs Altay | 2.03 | 3.44 | 3.44 |
| 20:30 | 3412 | Lazio vs Genoa | 1.43 | 4.72 | 6.83 |
| 22:00 | 1484 | Maastricht vs Emmen | 6.84 | 4.69 | 1.38 |
| 22:00 | 2129 | Santa Clara vs Vitoria Guimaraes | 3.16 | 3.31 | 2.19 |
| 22:00 | 2264 | Telstar vs Jong PSV | 2.50 | 3.43 | 2.55 |
| 22:00 | 3599 | ADO Den Haag vs NAC Breda | 2.01 | 3.55 | 3.26 |
| 22:00 | 4610 | VVV Venlo vs FC Oss | 2.11 | 3.48 | 3.09 |
| 22:00 | 4674 | Almere City vs FC Volendam | 2.83 | 3.61 | 2.20 |
| 22:30 | 1109 | Wisla Plock vs Lechia Gdansk | 2.51 | 3.29 | 2.51 |
| 22:30 | 3159 | FC Aarau vs Neuchatel Xamax | 1.77 | 3.85 | 3.61 |
| 22:30 | 4055 | Bayern Munchen vs VfL Wolfsburg | 1.17 | 7.59 | 12.98 |
| 22:30 | 4437 | FC Thun vs FC Schaffhausen | 2.00 | 3.61 | 3.08 |
| 22:30 | 4865 | Yverdon-Sport FC vs SC Kriens | 1.57 | 4.14 | 4.52 |
| 22:45 | 1065 | Glentoran Belfast vs Glenavon | 1.50 | 4.32 | 4.99 |
| 22:45 | 2602 | Larne vs Linfield Belfast | 1.99 | 3.42 | 3.27 |
| 22:45 | 2709 | Salernitana vs Inter | 13.93 | 6.96 | 1.18 |
| 22:45 | 2879 | Edinburgh City vs Forfar Athletic | 2.90 | 3.38 | 2.18 |
| 22:45 | 2897 | Cefn Druids vs Bala Town | 13.51 | 6.76 | 1.14 |
| 22:45 | 3637 | Barnsley vs West Bromwich | 4.51 | 3.48 | 1.75 |
| 22:45 | 5085 | Cardiff Met Uni. vs Barry Town FC | 1.83 | 3.56 | 3.66 |
| 22:45 | 5238 | Caernarfon Town vs Aberystwyth Town | 1.76 | 3.57 | 3.95 |
| 23:00 | 2549 | Paris FC vs Lyon | 5.75 | 4.56 | 1.47 |
| 23:00 | 4562 | Girona vs Burgos | 1.63 | 3.59 | 5.31 |
| 23:00 | 5295 | Celta Vigo vs Espanyol | 1.99 | 3.35 | 3.85 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Desemba 17, 2021

Nipashe



Arteta: Lacazette ameonyesha ukomavu

# NABI : HATUACHI KITU MSIMU HUU

## ●●●Kocha huyo asema ndio sababu kuu alipanga kikosi kamili katika...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema hakuna mchezaji yeyote ambaye ni 'staa' ndani ya timu hiyo na aliamua kupanga 'kikosi kamili' katika mechi ya Kombe la FA dhidi ya Ihefu SC kwa sababu hakuwadharau wapinzani hao kutoka Mbarali, Mbeya.

Yanga ilipata ushindi mnono wa mabao 4-0 na kusonga mbele katika mashindano hayo ambayo hutoa mwakilishi wa Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Nabi alisema hakutaka kubadilisha kikosi chake kwenye mechi hiyo kwa sababu aliwaheshimu Ihefu ambayo msimu uliopita ilikuwa inashiriki Ligi Kuu na ina historia ya kuwabana Yanga.

Kocha huyo alisema walijianda vizuri kwa ajili ya mchezo huo na wachezaji wake wamefanya kile alichowaelekeza mazoezini na kuwasisitiza kwamba katika timu yake hakuna mchezaji ambaye atakuwa juu na wote kuhakikisha wanapambania kutafuta matokeo.



Kiungo mshambuliaji wa Yanga, Jesus Moloko (kulia), akijaribu kumtoka mchezaji wa Ihefu katika mechi ya mashindano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 4-0. **PICHA: MTANDAO**

"Ni mechi niliyojiandaa kisawasawa, sikuidharau mechi hiyo kwa sababu Ihefu ni timu nzuri na msimu uliopita ilikuwa Ligi Kuu, si timu ndogo, imeshuka daraja lakini ni timu nzuri tu.

"Yanga ni timu kubwa na hakuna staa wa timu wala mchezaji mkubwa, kila mmoja ni muhimu na atapata nafasi kulingana na mahitaji yetu ya benchi la ufundi na kulingana na timu tunayoenda kukutana nayo," alisema Nabi.

Aliongeza baada ya kuwa na uhakika na ushindi ndipo alipoanza kubadilisha wachezaji, akiwaingiza wale ambao hawajacheza muda mrefu akiwamo, Yassin Mustapha ambaye kwa muda mrefu hajaonekana uwanjani kutokana na majeraha.

"Niliwapumzisha zaidi wachezaji ambao wametumika sana kwenye timu ya taifa na Ligi Kuu kama Dickson Job na Feisal Salum, nikawaingiza nyota ambao hawajacheza muda mrefu angalau na wao wapate muda wa kucheza, lakini ni baada ya kuwa na uhakika na ushindi," Nabi alisema.

Kuhusu, Shomari Kibwana ambaye aliumia katika mchezo dhidi ya Simba, kocha huyo amesema kutokana na majeraha yake, ataushauri uongozi kumpeleka nje ya nchi kwa ajili ya kupata matibabu bora.

Aliongeza kwa sasa wataendelea na mazoezi kwa ajili ya mechi yao ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayochezwa Jumapili dhidi ya Prisons.

"Kama nilivyosema awali malengo yetu makubwa ni kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo yetu ya Ligi Kuu na Kombe la FA, tumevuka katika mzunguko wa nne na sasa tunaenda kujiandaa na mchezo dhidi ya Prisons," aliongeza kocha huyo.

Naye Kocha Mkuu wa Ihefu, Zuberi Katwila, alisema 'hakuitolea macho' mechi hiyo kwa sababu malengo yake ni kupambana na kufanya vizuri kwenye Ligi ya Championship ambapo wako katika nafasi ya pili kwenye msimamo.

"Tulicheza michuano hii kwa sababu ni kanuni inatulazimu na tumepangiwa na Yanga, ilibidi lazima tucheze, lakini akili yetu ipo kwenye mechi za ligi, ndicho kipaumbele chetu, nikaamua kuchezesha wachezaji ambao hawachezi ili kuwalinda wachezaji wangu tegemeo," alisema Katwila.

**EDNA LEMA AREJEA**

Wakati Yanga ikiwa katika mchakato wa kunasa nyota wapya, kutoa wengine kwa mkopo, imetangaza rasmi kurejea kwa aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema.

Yanga pia inawatangazia wanachama na mashabiki wake katiba yao mpya ya mwaka 2021 iliyojadiliwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka imesajiliwa rasmi na serikali na kukamilika huko kunaruhusu utekelezwaji wa mabadiliko ya mfumo wa uendeshwaji wa klabu hiyo.

Katika taarifa yao ya jana, Yanga imesema iko kwenye mchakato wa kuwapeleka nje ya Tanzania wachezaji wao, Kibwana na Yusufu Athumani huku Fiston Mayele na Yacouba Songne afya zao zinaimarika zaidi.

## Simba SC yajiandaa kushusha majembe

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limefungua rasmi dirisha dogo la usajili, Klabu ya Simba imesema itafanya usajili wa kurekebisha kikosi chake kwa kuzingatia mwongozo utakaotolewa na Kocha Mkuu, Pablo Franco pamoja na benchi lake la ufundi.

Tayari tetesi zinasema nyota Moses Phiri kutoka Zambia ametua nchini kwa ajili ya kukamilisha mchakato wa kujiunga na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara.

Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu, amesema katika kipindi hiki wamepanga kujiimarisha kwa sababu wanahitaji kuona wanaendelea kufanya vizuri kwenye michuano mbalimbali wanayoshiriki.

"Tutafanya usajili wa kuboresha kikosi chetu, lakini hii itategemea na matakwa ya mwalimu wetu na benchi la ufundi, wao ndiyo watatuambia sehemu gani ina mapungufu na sisi tutawatekelezea," alisema Mangungu.

Simba ndiyo timu pekee iliyobaki kwenye mashindano ya kimataifa, ambapo wadau wa soka wameshauri kikosi hicho kinahitaji maboresho katika baadhi ya idara zake ikiwamo safu ya kiungo mshambuliaji ambaye atakuwa na uwezo kuichezesha timu.

TFF ilitoa taarifa ya kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili kwa ajili ya Ligi Kuu, Ligi ya Championiship, First League na Ligi Kuu ya Wanawake na dirisha hilo litafungwa ifikapo Januari 15, mwakani.

Shirikisho hilo pia limezitaka klabu zote kuheshimu kalenda hiyo iliyotolewa na watakaokuwa na changamoto yoyote wawasiliane na Idara ya Mashindano kwa ajili ya kupata ufumbuzi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >